# Nipashe

Ijumaa Novemba 10, 2023 • Tanzania 1000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581490

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




**CASEMIRO: NINAJUTA KUSAJILIWA UNITED**

UKURASA 22

**MAHAKAMA** yapewa somo ukubwa kosa kabla kutoa uamuzi

UKURASA 4



**WABUNGE** wamchangia Profesa Jay kusaidia wagonjwa wa figo

UKURASA 5



## Bei za petroli, dizeli, mafuta ya ndege Zanzibar zapaa

UKURASA 17

# Kikokotoo bado ni ngoma mbichi

**WALIMU** wamwangukia Rais Samia, aangalie kwa jicho la pili... *Endelea Ukurasa wa 2*



Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam, wakijipatia riziki kwa kuwakodisha mabuti na kuwaosha miguu watu wanaoingia na kutoka katika Soko la Mabibo, maarufu kama Mahakama ya Ndizi jana, kutokana na soko hilo kujaa tope lililosababishwa na mvua kubwa iliyonyesha siku chache zilizopita. Gharama ya kuosha na kukodisha buti ni Sh. 1,000. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UKURASA WA 2

## WABUNGE WASHAURI MBINU KATIKA KUUKABILI UMASKINI

WABUNGE wametaja mbinu za kupunguza tatizo la umaskini nchini, mojawapo ni serikali kujielekeza katika uwekezaji wa kilimo, uchimbaji wa gesi asilia, madini, uvuvi na utalii. Pia wameshauri ili kufanikiwa kupunguza umaskini ni lazima serikali idhibiti upotevu wa mapato, pamoja

## Polisi wataja chanzo kifo mke wa Askofu



UKURASA 2

## LATRA yabaini mchezo mchafu madereva mabasi safari za usiku

UKURASA 3

**MICHEZO** GAMONDI AFUNGUKA UBORA WA COASTAL UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi (kulia), akiagana na Naibu Katibu Mkuu wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola, Jarvis Matiya, baada ya mazungumzo yao, ofisini kwake Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Kikokotoo bado ngoma mbichi, walimu wamwangukia Samia

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

UMOJA wa Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania (TAPSHA), umewasilisha maombi kadhaa kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwamo kuangalia kwa jicho la pili kanuni mpya za ukokotoaji mafao (kikokotoo) ambayo imekuwa kilio kwa watumishi.

Juzi bungeni, Mbunge wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo, akiuliza swali, alihoji mpango wa serikali wa kufanya mapitio ya malipo ya mkupuo (kikokotoo) ya asilimia 33 kwa wafanyakazi.

Hata hivyo, Naibu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alijibu kuwa serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mafao ya pensheni ikijumuisha malipo ya mkupuo kwa wafanyakazi.

"Sheria inaitaka mifuko kufanya tathimini ya kupima uhimilivu kila baada ya miaka mitatu na kutoa ushauri na mapendekezo mbalimbali ikijumuisha maboresho ya mafao ya wanachama na kuifanya Mifuko kuwa endelevu,"alisema.

Alisema kwa kuwa mifuko itafanya tathmini kwa hesabu zinazoishia Juni 2023, serikali itazingatia ushauri wa mtaalam ambaye atafanya tathimini hiyo ili kuongeza pensheni ya wastaafu ambayo inajumuisha malipo ya mkupuo wa asilimia 33.

Katika mkutano huo jana, Mwenyekiti wa TAPSHA Umoja huo, Rehema Ramole alisema: "Kikokotoo kimekuwa kilio cha watumishi wengi. tunaomba utufikishie (Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Deogratius Ndejembi) kilio hiki kwa Rais Samia aangalie suala hili kwa jicho la pili."

Pia aliomba walimu wanaojitolea wapewe kipaumbele kwenye ajira zinapotolewa huku wakishauri somo la kiingereza lianze kufundishwa darasa la kwanza, ili kuwapa wanafunzi wepesi wafikiapo darasa la tatu na kuendelea.

Ramole alipongeza serikali kwa ujenzi wa miundombinu na jitihada za kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia. Akifungua mkutano huo, Ndejembi alitoa maagizo tisa kwa walimu wakuu wa shule za msingi nchini, ikiwamo kudhibiti matendo maovu na kuwalinda wanafunzi shuleni.

Alisema ni muhimu kushirikiana na wazazi, walezi na jamii inayozunguka shule, ili kulinda usalama wa wanafunzi na kuhakikisha wanadumisha mila desturi na utamaduni wa kitanzania kwa kuwafundisha wanafunzi historia ya Tanzania na kudhibiti matendo maovu yasitokee shuleni.

"Wakuu wa shule msimamie nidhamu ya walimu na wanafunzi shuleni wakati wote na kuhakikisha ulinzi wa mali za shule unaimarika wakati wote," alisema.

Aidha, aliwataka kusimamia miradi inayoendelea na itakayoletwa ili ikamilike kwa wakati, thamani ya fedha na miongozo iliyotolewa.

"Simamieni stahiki za watumishi wakiwemo walimu kama malipo ya fedha za likizo na kutenga bajeti za upandishwaji madaraja; kutenga muda wa kusikiliza kero za watumishi wote kwa lugha ya staha wakiwemo walimu ili kushiriki utatuzi wa changamoto zinazowakabili," alisema.

Pia alisisitiza kusimamia ufundishaji na ujifunzaji ili kuondoa tatizo la wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi bila kumudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu.

"Kusimamia na kuhamasisha jamii ili wanafunzi wote wapate huduma ya chakula shuleni, Wakuu wa Shule mnao wajibu wa kutambua na kuilinda mipaka ya shule ili kuondoa migogoro na jamii," alisema.

Ndejembi alisema wakuu wa shule wote mhakikishe mnasimamia ufundishaji wa stadi za KKK na lugha ya kiingereza kwa wanafunzi wote ili kuwajengea umahiri katika masomo yao.

# Wabunge washauri mbinu katika kuukabili umaskini

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WABUNGE wametaja mbinu za kupunguza tatizo la umaskini nchini, mojawapo ni serikali kujielekeza katika uwekezaji wa kilimo, uchimbaji wa gesi asilia, madini, uvuvi na utalii.

Pia wameshauri ili kufanikiwa kupunguza umaskini ni lazima serikali idhibiti upotevu wa mapato, pamoja na kuelekeza makusanyo ya kodi katika utoaji wa huduma za kijamii ikiwapo ujenzi wa hospitali, shule na upatikanaji wa majisafi.

Walieleza hayo jana wakati wakichangia Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25, pamoja na Mpango wa Taifa kwa Mwaka 2024/25.

Mbunge wa Musoma Vijijini (CCM), Profesa Sospeter Muhongo, alisema mpango wa maendeleo ni lazima ujielekeze katika kufuta umaskini.

Alisema kwa sasa hali ya umaskini nchini takwimu zinaonyesha asilimia 18.7 ya Watanzania wako katika umaskini na wanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa chakula.

Profesa Muhongo alisema asilimia 13 ya Watanzania anaoishi mjini ni masikini, asilimia 87 wanaoishi vijijini ni maskini.

"Uchumi wetu ni lazima ukue kwa asilimia nane hadi 10 maeneo ya kukuza huo uchumi kwanza ni uwekezaji katika gesi hususani gesi asilia, madini, uvuvi, kilimo, ufugaji na utalii.

Ni lazima tuwe na elimu bora katika ngazi zote kwa kupata walimu na wakufunzi walio bora, tupate vifaa bora kama vile maabara na vifaa vya kufundishia," alisema Prof. Muhongo.

Alisema pia mpango wa maendeleo ni lazima ujielekeze katika utafiti na ubunifu, kwamba hakuna taifa lililofanikiwa pasipo kufuata hayo maeneno.

Profesa Muhongo alisema Watanzania wanahitaji chakula, maji, umeme, matibabu, hivyo ni lazima mpango wa maendeleo uhakikishe unakwenda kutibu maeneo hayo.

Mbunge wa Namtumbo (CCM), Vita Kawawa alishauri kutengwa fedha za ziada kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya kielektroniki ili kudhibiti wizi.

Mbunge wa Kinondoni (CCM), Abbas Tarimba alishauri kuwekwa mifumo itakayowapa taarifa wafanyabiashara kutambua kiasi cha kodi wanachotakiwa kutozwa, ili kuepuka malalamiko ya kutozwa kodi kubwa.

Mbunge wa Geita (CCM), Joseph Kasheku alisema kumekua na upangaji wa mipango kwa miaka mingi lakini utekelezaji wake umekua ukisuasua.

# Polisi wataja chanzo kifo mke wa Askofu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Geita limetegua utata kuhusu kifo cha Monica Vithalis, Mke wa Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Biharamulo, Mhashamu Vithalis Yusufu.

Taarifa ya jeshi hilo imebainisha kuwa mke wa kiongozi huyo wa kiroho katika kanisa ambalo ni la tatu kwa ukubwa nchini, hakuuawa kama ilivyokuwa imedaiwa mwanzo bali alijinyonga kutokana na msongo wa mawazo na maradhi yaliyokuwa yakimkabili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Askofu Mkuu wa Kanisa Anglikana Tanzania, Dk. Maimbo Mndolwa, mwili wa Monica ulikutwa umetelekezwa kando ya barabara kwenye msitu ulioko Kijiji cha Kusega wilayani Chato, mkoani Geita ukiwa na kamba shingoni juzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi (ACPO Safia Jongo, akizungumza kwa simu jana, alisema Monica hakuuawa bali alijinyonga kwa kamba katika moja ya miti iliyoko katika msitu kwenye kijijini hicho.

Alisema Jeshi la Polisi lilifika katika eneo la tukio na kumkuta mama huyo akiwa amening'inia katika mti kisha kumtoa na kwenda kumfanyia uchunguzi wa kitabibu kwenye Hospitali ya Rufani ya Kanda, Chato na kubaini kuwa alijinyonga.

Kuhusu sababu za kujinyonga kwake, Kamanda Jongo alisema jeshi hilo lilimhoji mume wa marehemu, Askofu Yusufu, ambaye alisema mke wake alikuwa na mawazo kutokana na kusumbuliwa kwa muda mrefu na saratani.

"Kilichotekea ni kwamba huyu mama ni mgonjwa na amefanyiwa upasuaji mara mbili lakini aliendelea kusumbuliwa na ugonjwa wa saratani, hivyo kumuomba mume wake ampeleke kwa mganga wa kienyeji. Wakati akimpeleka, alimwachia njiani ili aendelee na safari.

"Askofu huyo alimwacha njiani kwani alikuwa akiwahi katika shughuli zake na akimaliza ataenda kumrudisha lakini hakumrudia ndipo alipokutwa porini akiwa amejinyonga," alisema Kamanda Jongo.

Kutokana na kifo hicho, Kamanda Jongo alisema jeshi hilo halimshikilii mtu yeyote kkwa kuwa hakuna sehemu yoyote iliyobainisha kuwa aliuawa bali alijiua kutokana na msongo wa mawazo kutokana na maradhi ya saratani na pumu.

"Uchunguzi wa eneo la tukio pamoja na madaktari wa Hospitali ya Rufani Chato zimethibitisha kabisa kuwa Monica hajauawa na mtu yeyote bali amejiua kwa kujinyonga. Asingefariki (dunia) tungeshughulika na yeye kwa kujaribu kujiua," alisema.

Kamanda Jongo alisema baada ya vipimo na uchunguzi, mwili huo tayari umehamishiwa katika Hospitali Teuli ya Wilaya ya Biharamulo kwa ajili ya taratibu zingine za kifamilia.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Moravian la Uamsho Tanzania, Emmaus Mwamakula, katika ujumbe wake wa pole kwa kanisa hilo, kabla ya taarifa rasmi ya polisi, alieleza kusikitishwa na tukio hilo huku akiomba serikali kufanya uchunguzi kuhusu vifo vya watumishi wa kanisa vinavyoendelea katika maeneo ya Kanda ya Ziwa.

Desemba, mwaka jana, mwili wa Askofu Mstaafu wa Kanisa Anglikana Dayosisi ya Victoria Nyanza, Boniface Kwangu, ulikutwa ukielea katika Ziwa Victoria karibu na daraja la Kigongo-Busisi, maarufu kama daraja la JPM huku serikali ikieleza kufanyia uchunguzi.

## HABARI KITAIFA



Wananchi wakishiriki kuchimba kaburi kwa ajili ya maziko ya marehemu Leah Lupasio, mkazi wa kitongoji cha Makang'wa, wilayani Mvomero, mkoani Morogoro juzi, aliyeuawa kwa Tembo mapema wiki hii, wakati akiokota kuni jirani kidogo na nyumbani kwake. **PICHA: IDDA MUSHI**.

# LATRA yabaini mchezo mchafu madereva safari za usiku

**Na Elizabeth Zaya**

KWA kipindi cha mwezi mmoja tangu kuruhusiwa kwa safari za usiku, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imebaini baadhi ya madereva kuchezea kifaa cha kudhibiti mwendo (VTS) na kuendesha mwendokasi.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema katika kipindi hicho cha mwezi mmoja walioruhusiwa safari za usiku, kati ya 246, madereva 110 walibainika kutotumia mfumo wa utambuzi wa dereva (i-button), huku mabasi 197 yakibainika kwenda mwendokasi kati ya kilomita 86 hadi 89 kwa saa na asilimia tisa wakiendesha mwendokasi kati ya kilomita 90 hadi 103 kwa saa.

Kadhalika, Suluo alisema kwa ratiba zote za safari za mabasi ikiwamo za usiku, walikamata mabasi 759 yaliyobainika kwenda mwendokasi pamoja na kuchezea mfumo na tayari wamechukua hatua ikiwamo kusitisha leseni kwa mabasi 36 huku madereva 10 wakifungiwa leseni kwa kuchezea mfumo huo wa VTS.

Alisema madereva 666 waliandikiwa faini kwa makosa ya kuendesha mwendokasi, 50 walionywa na 32 wamefikishwa mahakamani.

Suluo alisema kampuni zilizoongoza katika kuchezea mfumo wa VTS na mwendokasi ni ya Kapricon ambayo mabasi yake tisa yamefungiwa ikifuatiwa na Abood mabasi mawili na Dar Exepress mabasi mawili huku kampuni 23 kila moja zikifungiwa gari moja moja.

"Tathmini inaonyesha kuna mahitaji makubwa ya safari za usiku na imechangia kwa kiwango fulani kurahisisha michakato ya shughuli za kiuchumi, lakini katika kufuatilia tumebaini kwamba suala la VTS bado kuna shida kubwa ya kuichezea, kuna magari hayatoi taarifa kabisa na kuna yanayotoa taarifa kwa kurukaruka na mengine hayatoi kabisa," alisema Suluo.

"Kwahiyo wanachezea mfumo ili gari zisionekane. Tumewapa nafasi ya mwisho wajirekebishe kwa sababu wakiendelea kufanya hivyo sisi ndio tutawasha VTS na kuunganisha moja kwa moja kwenye faini kwa gari zitakazokwenda mwendokasi. Sisi kama LATRA tumependekeza huu utaratibu uanze Desemba, mwaka huu na kabla ya kufika huko tutazungumza na wamiliki wa mabasi."

Suluo alisema wanatarajia kuanza kutumia mfumo wa moja kwa moja wa kielektroniki wa kutoa faini kwa mabasi yanayokiuka sheria za barabarani hususani kuendesha kwa mwendokasi ili kudhibiti ukiukwaji huo wa sheria za barabarani.

Alisema wakiwasha mfumo huo wa kutoza faini moja kwa moja kielektroniki, watajadili faini ipi itumike kati ya Sh. 50,000 au 30,000 kwa kosa moja na kwamba mfumo huo kiwango chake cha mwisho kwa siku ni Shilingi milioni moja endapo dereva ataendelea kufanya makosa hayo.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Ramadhani Ng`anzi, alisema hawatafumbia macho madereva wote wanaokiuka sheria za barabarani na watakuwa wanaweka hadharani majina na picha za madereva wote wanaositishiwa leseni zao kwa makosa ya barabarani.

Alisema madereva wote waliositishiwa leseni zao watapaswa kufanya mtihani upya na watarejeshewa endapo watafaulu mitihani hiyo na kwa watakaoshindwa watawashauri kwenda vijijini wakaendeshe magari yasiyohitaji leseni hiyo.

"Tumefurahi kwamba tunakamilisha mazungumzo, tukianza kutumia mfumo wa kielektroniki wa moja kwa moja wa faini utasaidia kudhibiti madereva wasiofuata sheria," alisema Kamanda Ng`azi.

Katibu Mkuu wa Chama cha Mamiliki Mabasi Tanzania (TABOA), Priscus Joseph, aliiomba LATRA kuwapa majina ya madereva wote wanaokwenda kinyume na sheria za barabarani.

"Tumekuwa tukiomba miaka mingi sana turuhusiwe kwenda safari za usiku, leo hii tumeruhusiwa, lakini tunataka tena kuharibu sisi wenyewe, tunaomba na sisi tushirikishwe, tupewe majina ya hao ambao hawataki kufuata sheria," alisema Joseph.

Akizungumzia mchakato unaoendelea wa marejereo ya nauli mpya, Mkurugenzi wa LATRA alisema, matokeo ya kilichoamuliwa kuhusu nauli hizo yatatoka wakati wowote kuanzia mwezi huu na kwa sasa umefikia kwenye hatua ya serikali.

# Agizo RC laleta mabadiliko usafiri treni daladala Dar

**Na Mwandishi Wetu**

SAA 24 tangu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, kukagua madhila ya usafiri wa treni daladala kati ya Gerezani na Pugu na kutoa maelekezo kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC), mabadiliko mengi ya maboresho yamefanyika.

Gazeti hili limeshuhudia hali hiyo upande wa pili katika Barabara ya Nyerere, ambako nako kuna maelekezo kwa makandarasi wanaojenga miundombinu ya usafiri wa mwendokasi, jambo ambalo lilichangia foleni ya magari na treni kutokana na kuelemewa, hasa kipindi cha mvua.

Juzi asubuhi, kabla ya kuondoka Stesheni ya Reli Gerezani, Chalamila aliagiza mambo mawili, mosi, TRC ichukue hatua dhidi ya malalamiko yaliyotolewa na pili, Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Dar es Salaam imfahamishe mkandarasi kuhusu maboresho ya barabara.

Jana asubuhi, Nipashe ilishuhudia kutoweka kwa foleni za magari kwenye Barabara ya Nyerere, tofauti na siku mbili zilizopita ambazo magari yalikuwa na foleni kubwa kati ya Buguruni hadi TAZARA na Ukonga.

Uchunguzi wa Nipashe ulibaini mkandarasi katika Barabara ya Nyerere alitekeleza agizo la Mkuu wa Mkoa kupitia TANROADS, barabara zikawa zimetanuliwa kuwezesha magari kupita kirahisi licha ya wakazi kusema Ukonga kulinyesha mvua usiku wa manane, hivyo kusababisha foleni.

Pia yalishuhudiwa mageuzi makubwa ndani ya treni, baada ya mwandishi wa habari hii, aliyetumia usafiri huo asubuhi kati ya Gerezani na Pugu na kurejea, kuona abiria wakipewa nafasi kubwa kusikilizwa maoni yao.

Katika treni pia kulikuwapo matangazo kuhusu maboresho ya safari ambayo yameanzishwa saa 4.30 asubuhi kutoka Gerezani na kurejea saa 6. 30 adhuhuri.

Vilevile zimeongezwa safari mpya tatu kwa siku za Jumamosi, mbili asubuhi kati ya saa 2.00 asubuhi na saa 5.00 huku jioni ikiwapo moja inayoanza safari Gerezani saa 11.00 jioni.

Juzi, akitoa ufafanuzi wa malalamiko ya umma, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Amina Lumuli, alisema siku za wikiendi zimepangwa kwa ajili ya matengenezo ya treni.

Wakati treni inaendelea, wakatatisha tiketi walionyesha umakini dhidi ya kashfa iliyoibuliwa ya kuuza tiketi mara mbili. Jana, hali ilikuwa tofauti kwa kuwa abiria walipofika mwisho walihakikisha tiketi zote za safari zinachanwa.

Aidha, wakati treni ikifanya safari kwenda Pugu, baadhi ya mabehewa yalifungwa milango kwa madai kuwawekea nafasi wanaopanda stendi ya mwisho Pugu, hali iliyoibua malalamiko na mara moja hatua ilichukuliwa kwa kutolewa tangazo kuagiza mabehewa yote kufunguliwa milango yote, kuwezesha abiria waliosimama kukaa.

Hilo ni jambo ambalo siku kadhaa nyuma haikuwezekana na kuna wakati ilisababisha mizozo kati ya abiria na polisi.

Miongoni mwa kasoro zingine zilizotolewa juzi ni kukosekana chumba cha wasiojiweza, upungufu mabehewa ya wanafunzi kukosekana huduma ya choo kwenye treni, feni na lugha chafu dhidi ya abiria zinazotolewa na polisi na wafanyakazi wa TRC.



Ofisa Uangalizi Mfawidhi wa Ofisi ya kusimamia utekelezaji wa adhabu mbadala wa kifungo gerezani mkoa wa Iringa, Hamis Jengela (kulia), akionyesha kitabu cha mwongozo wa kishería kwa wafungwa wanaostahili adhabu mbadala, wakati akizungumza na mwandishi wa gazeti hili, Francis Godwin jana, kuhusu mjane Maria Ngoda aliyefungwa miaka 22 kwa kosa la kukutwa na vipande 12 vya nyama ya Swala. **PICHA: SELEMAN YUSUPH**

# Mshtakiwa akana kuhusika mauaji dada Bilionea Msuya

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA namba mbili katika kesi ya mauaji ya dada wa aliyekuwa mfanyabiashara wa madini Arusha, Erasto msuya, maarufu kama Bilionea Msuya, Aneth Msuya, Revocatus Muyela (48), amekana kuhusika na mauaji hayo na kusisitiza kuwa tuhuma hizo ni za uongo.

Aidha, Muyela ameyakataa majina yaliyomo kwenye hati ya mashitaka (Revocatus Everist Muyela a.k.a Revo/Ray) na kudai si majina halisi na mtu huyo hamfahamu. Amedai kuwa kwenye cheti chake cha kuzaliwa, majina yake halisi ni Revocatus Everest Patrick Muyela.

Muyela katika kesi hiyo ya mauaji namba 103 ya mwaka 2018, anashtakiwa pamoja na aliyekuwa mke wa Bilionea Msuya, Miriam Mrita, kwa madai ya kumuua Aneth.

Mshitakiwa huyo alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, wakati akitoa utetezi wake kama shahidi wa tano wa upande wa utetezi, akiongozwa na Wakili Nehemiah Nkoko.

Muyela alidai kuwa tuhuma kwamba alimchinja Aneth hadi kufa ni za uongo kwa sababu Mei 25, 2016 hakutoka kabisa nje ya mkoa wa Arusha na kwamba siku hiyo alikuwa akiendelea na shughuli zake.

Pia alidai kuwa hakuwahi kushirikiana na Mrita kumuua Aneth kwa sababu hajawahi kufika Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam kunakodaiwa kutokea tukio hilo.

Baada ya Wakili Nkoko kumrudisha shahidi kuelezea majina yake halisi, Muyela aliomba mahakama ipokee cheti hicho kama kielelezo pamoja na hati ya kusafiria inayoonyesha majina hayo.

"Hati yangu ya kusafiria ilitolewa Juni 8, 2012 na muda wake wa kuisha ilikuwa ni Juni 7, 2022 na mimi nilikamatwa Oktoba 19,2016. Kwa hiyo kuanzia hapo sijawahi kuwa huru kwenda kuomba hati nyingine. Naomba mahakama ipokee kama kielelezo," alidai Muyela.

Jaji Kakolaki alipokea vielelezo hivyo kama DE 12 na DE 13. Alifikia uamuzi huo baada ya upande wa mashitaka na wakili wa mshitakiwa wa kwanza, Peter Kibatala kutokuwa na pingamizi.

Pia alidai kuwa hakukamatwa kwa sababu Koplo Abdallah au Dulla alimwomba lifti kutoka katika eneo lake la kazi, yaani ofisi za Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Arusha na kumpeleka Kituo Kikuu cha Polisi ambako sio mbali na eneo hilo.

"Nilipofika alishuka na ghafla kuna gari ikanizunguka nyuma. Nilimwona ASP Omary Mahita akishuka kwenye hilo gari akaja kwangu kunieleza kuwa niko chini ya ulinzi, wakanipekua maungoni kisha walinipeleka mahabusu.

"Walichukua simu zangu tatu, pochi ambayo ndani yake kulikuwa na Dola za Marekani 450 na Sh 60,000, wakaniweka mahabusu. Baada ya hapo hakuna kilichoendelea cha upelelezi," alidai.

Alidai kuwa alipomuuliza Mahita kuwa anatuhumiwa na nini, alimweleza kwamba hata yeye hajui na kwamba alipigiwa simu na bwana anayetoka Dar es Salaam kwa hiyo akifika ndipo atamueleza makosa yake.

"Bwana huyo alifika ambaye ni mpelelezi mkuu wa hii kesi, ASSP David Mhanaya. Alijitambulisha kwangu kuwa anatoka Makao Makuu Dar es Salaam nami nilijitambulisha kwake akaniambia ninatuhuma zangu Dar es Salaam kwamba nimeshirikiana na Miriam kumuua Aneth," alidai .

Alidai kuwa ASSP Mhanaya alimuuliza Mei 15, 2016 alikuwa wapi? Akamweleza kwamba alikuwa nyumbani kwake Burka, Arusha na kwamba siku tatu zilizopita alipata wageni nyumbani baada ya mke wake kujifungua mapacha.

"Tarehe 20/8/2016, ASP Mhanaya na Koplo Hassan walikuja Kituo cha Polisi wakanichukua tukaanza safari ya kuja Dar es Salaam. Tulifika usiku, kesho yake ndiyo nilijua kwamba nipo Kituo cha Polisi Buguruni," alidai.

Kuhusu ushahidi wa ASP Mhanaya kwamba walipekua nyumbani saa 4:00 usiku, alikanusha na kusisitiza hakuwahi kumpeleka mtu nyumbani kwake na hata kwenye hati ya upekuzi sahihi iliyokuwapo si yake bali iliyokuwamo kwenye hati ya kusafiria ndiyo sahihi.

Pia alidai kuwa bastola ambayo inadaiwa ilikutwa nyumbani kwake si kweli kwa sababu ni mali ya Revocatus Everist Mollel mwenye anuani ya Ilala Bomani, Dar es Salaam na yeye anaishi Arusha.

Alidai kuwa baada ya hatua hiyo, hakuna hatua yoyote ya upelelezi iliyoendelea hadi tarehe 2/9/2016 aliyopelekwa Mahakama ya Kisutu, hivyo hakuwahi kutoka Kituo cha Polisi Buguruni kwenda sehemu yoyote.

Kuhusu gwaride la utambuzi, alidai kuwa hajawahi kufanyiwa. Kwa mujibu wa nyaraka, aliyefanyiwa gwaride ni Revocatus Everist na hata Saini iliyoko kwenye kielelezo hicho, haina uhusiano naye kabisa.

Kuhusu ushahidi uliotolewa kwamba alichukuliwa mateka kwa ajili ya vipimo vya vinasaba (DNA) vinavyohusishwa na kisu kilichokutwa eneo la tukio, alidai si kweli kwa sababu hakuwahi kutoka Buguruni kwenda sehemu yoyote.

Alidai kuwa aliwasilisha mahakamani nyaraka kupinga tarehe 15,18,20,23 na 25/5/2016 ambazo anatuhumiwa alikuwa Dar es Salaam na pia aliomba simu zake tatu na maelezo yake ya onyo, Lakini hadi shahidi wa 25 anamaliza kutoa ushahidi, hakuwahi kupewa.

"Nilitaka simu ili nizitumie kuthibitisha kwamba nilikuwa Arusha. Sikutoka kwa sababu minara ingeonyesha na maelezo ya onyo. Nilitaka nithibitishe kwamba sikukiri kwa polisi kama niliua na pia mawasiliano yangeonekana kati yangu na Miriam," alidai.

Pia alidai kuwa wangeangalia kwenye simu hizo kama kuna maudhui ambayo yalikuwa na nia ovu na pia hakuna shahidi hata mmoja aliyedai kuwa alimwona wakati anamuua Aneth wala ndugu wa marehemu hawakuthibitisha.

Baada ya kumaliza kutoa ushahidi wake, aliiomba mahakama ipime ushahidi uliotolewa kama anahusika au hahusiki imwachie huru akaungane na familia yake. Kesi hiyo iliahirishwa hadi leo kwa upande wa utetezi kuendelea na ushahidi.

Miriam mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji hayo ya wifi yake, Aneth, anayedaiwa kuuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada, Dar es Salaam, alikiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo.

# Korti yapewa somo ukubwa wa kosa kabla kutoa uamuzi

**Na Francis Godwin,**
IRINGA

MAHAKAMA zimeshauriwa kuangalia mawanda ya sababu na vigezo kabla ya kutoa hukumu kulingana na kosa na pia kutoa hukumu kwa matakwa na kwa mujibu wa sheria na aina ya mtu aliyepatikana na hatia.

Hali hiyo imeelezwa kuwa hata misingi ya viwango vya kimataifa, inasema mtu anapotiwa hatiani moja ya mambo yanayopaswa kuangaliwa ni kuangalia hali ya mtu aliyekosa ili kumrekebisha na kuwa mwema katika jamii.

Hayo yalisema na Ofisa Uangalizi Mfawidhi wa Mkoa wa Iringa, Hamis Jengela, Akizungumza katika mahojiano maalumu na Nipashe jana ofisini kwake mjini hapa,

Alisema ofisi yake inashughulika na utekelezaji wa adhabu mbadala wa kifungo gerezani huku akibainisha kwamba uwezo wao ni kumsaidia mtu aliyefungwa kifungo cha miaka isiyo zidi mitatu. Kutokana na hali hiyo, alisema ni vigumu kwa mtu kama Maria Ngoda aliyefungwa miaka 22 baada ya kupatikana na hatia ya kukutwa na vipande 22 vya nyama ya swala.

Alibainisha kuwa katika utendaji wao wa kazi, wamewahi kuwasaidia waliofungwa kwa kuua bila kukusudia na wale walibainika kuwa na makosa ya kuingia hifadhini kinyume cha sheria.

Kwa mujibu wa Jengela, ili kupata msaada wa huduma za kijamii, ni lazima ombi litoke gerezani kwa mkuu wa gereza na ofisi yake inakwenda kufanya uchunguzi kwenye jamii ili kujua kama kuna madhara yoyote ya mhusika iwapo atapewa adhabu mbadala.

Hata hivyo, Jengela alisema mahakama inapaswa kuangalia sana kabla ya kumtia hatiani mtu anayekosa kwa kuangalia hitaji la marekebisho na pia hazifikirii kwa kina sana katika kutoa adhabu kwa wakosaji.

"Ni sahihi sana inapofika hatua kwa kutoa adhabu kufikiri ili kuangalia adhabu sahihi ambayo itakuwa hailengi ukubwa wa kosa bali kumrekebisha mtu kuwa raia mwema na si kumkomesha," alisema.

Kuhusu mtazamo wa wengi juu ya kesi ya Malkia ya Pembe za Ndovu aliyekutwa na vipande 511 vya meno ya tembo kupigwa faini, alisema hapo ndipo anapojiuliza mahakama Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam ilitazama nini na Mahakama ya Iringa iliangalia nini hadi kutoa adhabu ya kifungo jela miaka 22.

Alisema wakati mwingine kwenye utekelezaji wa sheria na uamuzi, huwa kuna mitazamo tofauti kwa watoa haki japo asingependa kushutumu mahakama zote.

Pamoja na hayo, alisema ni vyema kuangalia kwa kina namna ya utoaji wa adhabu kwak uwa sheria inalenga kumwadhibu, kumrekebisha au kumwonya mkosaji na kwamba hivyo vyote vinawezekana.

Alisema kuwa kumekuwa na mitazamo tofauti kati ya kesi ya pembe za Ndovu 511 na adhabu iliyotolewa na nyama ya Swala vipande 12 kuwa na adhabu kubwa zaidi

Jengela alisema tasngu amekuwapo katika ofisi hiyo, amejifunza kuwa kwa sehemu sheria imekaa vyema na sehemu pia haiku hapo vizuri. Kwa upande wa kulinda rasilimali za taifa, anaona sheria imekaa vizuri na vyema jamii ikaepuka kufanya makosa ya ujangili. Jengela pia alisema bunge limetunga sheria nzuri ya dhidi ya ujangili na uhujumu uchumi lakini watendaji wa mahakama wanayo nafasi ya kuboresha sheria.

Sakata la Ngoda, mjane na mama wa watoto wanne, limeendelea kuchukua sura mpya kwa jamii kuonesha nia ya kumsaidia. Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) kupitia mwenyekiti wake, Mary Chatanda, umejitokeza kutaka kumsaidia kwa kuweka mwanasheria kukata rufani dhidi ya adhabu hiyo.

Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) Mkoa wa Iringa pia kimejitokeza kumsaidia mjane huyo pasipo gharama kwa kupanga mawakili 10 ambao watafanya kazi ya kumtetea mahakamani baada ya kukata rufani.

Aidha, Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Iringa, Joseph Lyata, alisema chama mkoa kimejipanga kufuatilia familia ya mjane huyo ili kuona namna ya kuisaidia, ikiwamo kumwezesha mmoja wa Watoto wake kuendelea na masomo ya sekondari.

Ngoda alihukumiwa Novemba 3, mwaka huu na Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Iringa, Said Mkasiwa, baada ya kujiridhisha kuwa ni kweli mjane huyo, alikutwa na ndoo iliyokuwa na nyama ya swala yenye thamani ya Sh 900,000 kinyume cha sheria .

**HABARI KITAIFA**




Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle (kulia), akijadiliana jambo na baadhi ya washiriki wa mkutano wa sekta binafsi ya Marekani na Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Tanzania yashauriwa kuimarisha sekta binafsi kukuza uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Marekani nchini Michael Battle, amesema Tanzania imefanya mambo mengi ya muhimu kuboresha sera na mazingira ya biashara hatua itakayoifikisha mbali.

Alisema hayo katika mkutano wa majadiliano ya pamoja kati ya Marekani na Tanzania ulioandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI) kwa kushirikiana na Baraza Kuu la Biashara la Afrika (CCA) Corporate Council of Africa (CCA).

Balozi Battle alisema Tanzania inatakiwa kuendelea kuijenga sekta binafsi kuwa imara zaidi kwa kuwa ni kiungo muhimu katika ujenzi wa uchumi hasa kutengeneza ajira nyingi kwa watu wake.

Alisema kama Tanzania inataka kutimiza malengo yake kwa kiwango kikubwa, inabidi izidi kuweka mazingira wezeshi yatakayoimarisha sekta binafsi na kuzalisha ajira nyingi zaidi kwa watu wake.

Balozi Battle alisema kuwa Marekani na Afrika zinafanya kazi kwa muda mrefu, changamoto ni kwenye ubora wa bidhaa na kushauri ni vyema wafanyabiashara wakapata elimu ya kutosha ya ubora wa bidhaa zinazotakiwa kuuzwa Marekani.

Pia, alisema Marekani inatumia fedha nyingi kutoa misaada ya kijamii katika nchi za Afrika hasa Tanzania na imefika wakati sasa kuipunguza na kuelekeza nguvu zaidi katika miradi ya uwekezaji na uchumi.

Balozi Battle alisema itasaidia jamii ya kitanzania kwenye upande wa kujikwamua kiuchumi kwa kuwa wananchi ndio watakaozalisha na kufanyabiashara hizo ziwe rasmi na madhubuti kati ya nchi hizo mbili.

Rais na Mtendaji Mkuu wa CCA (Corporate Council of Africa (CCA), Florie Liser, alisema nia ya mkutano huo ni kuhamasisha uhusiano uliopo kati ya Tanzania na Marekani.

"Tanzania ni nchi ambayo inapewa kipaumbele kunufaika na fursa zilizopo katika soko la AGOA, ambapo mkataba umesainiwa kati ya Serikali ya Tanzania na Marekani ili kuboresha mazingira ya biashara kati ya nchi hizi mbili, na mkutano hii inaashiria mwanzo mwema hivyo itakuwa endelevu kwa jinsi siku zinavyoenda," alisema.

Kadhalika, alisema Tanzania inanufaika na soko la AGOA na kutoa mfano wa kiwanda cha Tanzania Tooku Garment cha Dar es Salaam ambacho kimeajiri watu zaidi ya 3,500 wengi wao ni wanawake.

Alisema baada ya janga la Corona, viwanda vingi vinatafuta sehemu za kuwekeza miradi yao sehemu tofauti ili uzalishaji wa bidhaa usiathiriwe sehemu moja na hasa inapopatwa na majanga.

Liser alisema Afrika imekuwa bara ambalo wawekezaji wengi wanapafikiria na kuitaka Tanzania kutumia fursa hiyo vizuri.

Balozi wa Tanzania nchini Marekani, Dk. Elsie Kanza, alishukuru juhudi zinazofanywa na Serikali ya Marekani kuboresha mazingira ya biashara na uungawaji mkono kutoka Serikali ya Tanzania katika juhudi za kuboresha mazingira ya biashara.

Pia, mkutano wa mwezi huu wa AGOA utakaofanyika Afrika ya Kusini unaonyesha juhudi ambazo Bara la Afrika linafanya katika kuimarisha diplomasia ya uchumi kati yake na Marekani.

Alisema Tanzania inaweza kutumia USA kama njia ya kupitishia bidhaa zake kwenda nchi za jirani na Marekani ili kunufaika na fursa zilizopo na Mfanyabiashara anaweza kuanza kidogo na kuendelea kukua kwa kujenga imani kwa wateja.

Meneja wa Uhamasishaji Uwekezaji wa Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), Panduka Yonazi, amesema Tanzania kupitia Programu ya EPZ ina viwanda vinavyouza nguo aina ya jinsi, fulana na nguo za watoto katika soko la Marekani kwa asilimia 100.

Viwanda hivyo vimeajiri zaidi ya watu 7,000 ambavyo ni Tanzania Tooku Garment cha Dar es Salaam, Mazava Fabrics cha Morogoro na Red Earth cha Arusha.

Pia EPZA imeendelea kuhamasisha jamii ya wafanyabiashara wa kimataifa na wazawa kutumia fursa za uwekezaji ambazo serikali imeziweka na kunufaika na vivutio pamoja na uwezeshaji wa biashara unaotolewa na EPZA.

# Wabunge kuchangia taasisi ya Profesa Jay kusaidia wagonjwa figo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



WABUNGE wameungana kumchangia Mbunge wa zamani wa Mikumi na msanii wa Bongo Fleva, Joseph Haule (Profesa Jay) (pichani) ili kuunga mkono taasisi yake anayoanzisha ya kusaidia wagonjwa wa figo.

Profesa Jay, alikwenda bungeni jana akiwa mmoja wa wageni waalikwa kwenye jukwaa la Spika na kutambulishwa na Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson.

Dk. Tulia alisema kuna ugeni wa viongozi watatu wa taasisi ya Profesa Jay, ambayo inatarajia kuzinduliwa Novemba 24, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

"Pia kwa kuzingatia kuwa amesimama kwa ushuhuda kuwa alipata changamoto hii na madaktari walijitahidi kumpa matibabu, tuna mshukuru Mungu kwa uponyaji wake na tunakutakia kila la heri kwa taasisi yako," alisema.

Baada ya kutangaza, wabunge wawili, Geita Vijijini, Joseph Musukuma (CCM) na Nkasi Kaskazini, Aida Khenani (Chadema), walisimama kuomba mwongozo wa Spika kama wanaruhusiwa kuchangia taasisi hiyo.

Mbunge Khenani aliomba mwongozo wa Spika kama inaruhusiwa kila mbunge kuichangia taasisi hiyo Sh. 50,000.

Mbunge Musukuma alisimama na kuomba mwongozo wa Spika, akisema: "Kwa kuwa kiongozi wa taasisi hii alikuwa mbunge mwenzetu, na kwa kuwa yeyote miongoni mwetu anaweza kupitia changamoto kama hii, naomba mwongozo kama kila mbunge anaweza kuchangia Sh. 200,000 ili Sh. 100,000 iwe kwa ajili ya Profesa Jay na Sh. 100,000 ielekezwe kwenye taasisi."

Kutokana na miongozo hiyo, Spika Tulia alielekeza wabunge kuchangia ndani ya siku mbili kuanzia jana.

Katika siku za karibuni, Profesa Jay alionekana kwenye mitandao ya kijamii, akielezea gharama kubwa za kutibu maradhi ya figo huku akitoa ushuhuda fedha zilizotumika kumtibu.

Alisema kwa watu wasiokuwa na uwezo wa kulipia gharama hizo wengi wanapoteza maisha na kwamba lengo la kuanzisha taasisi hiyo ni kuwasaidia watu wasioweza kumudu gharama hizo.

The United Republic of Tanzania
President's Office

09.11.2023

VACANCY ADVERTISEMENT

EXTENSION OF DEADLINE FOR SUBMISSION

Tanzania Social Action Fund (TASAF) is currently implementing Productive Social Safety Net Program which aims at protecting the Vulnerable Poor Households from severest consequences of poverty by implementing interventions that will lead to increased Household incomes and opportunities while increasing consumption.

The Permanent Secretary, President's Office, State House advertised a vacant post for TASAF Executive Director from 10th October 2023 and the deadline was 10th November 2023.

The general public is hereby informed that the deadline for submission has been extended from 10th November 2023 to 27th November 2023.

All other details remain as they were advertised in the original invitation.

PERMANENT SECRETARY
PRESIDENT'S OFFICE, STATE HOUSE

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jamii ielimishwe kutambua watoto wenye Usonji

**BALOZI** wa Australia nchini, Luke Willliams amenukuliwa na vyombo vya habari likiwamo gazeti hili akisisitiza kuwa jamii inapaswa kupatiwa elimu bora ya kuwatambua watoto wenye ugonjwa wa Usonji ili waweze kuondokana na vitendo vya unyanyapaa na unyanyasaji wanavyokumbana navyo nchini na duniani kote.

Balozi Willliams amenukuliwa hayo katika uzinduzi wa katuni mpya iitwayo FIDI kwa kushirikiana na Kituo cha Kutibu Watoto cha Gabriella Rehabilitation Center kwa kutumia watu hai wenye Usonji, familia na marafiki zao, inayoelezea jinsi ya kuwatambua watoto na vijana wenye tatizo hilo na kuwapeleka vituo vya afya au vituo maalumu vya kulelea watoto wenye ugonjwa huo na mengine.

Jamii inapaswa kuelewa kuwa watoto wenye tatizo hilo ni kama wengine, hivyo wanastahili kupendwa na kupatiwa mahitaji muhimu ikiwa ni pamoja na afya, chakula na elimu kwani ni msingi wa maisha yao ya baadaye badala ya kuwatelekeza ikiamini kuwa hawana faida wala msaada wowote.

Watoto hao kama walivyo wengine, endapo watagundulika mapema na kupatiwa matibabu na elimu, wanauelewa mkubwa kama inavyoelezwa na wataalamu wa afya.

Wataalamu wanasema Usonji ni ugonjwa wa vinasaba kutoka kwa wazazi wa mtoto, hivyo mara anapozaliwa, madaktari wanapaswa kumfanyia uchunguzi wa kina ili kubaini mapema tatizo hilo na kuanza kumpatia matibabu kwa sababu ugonjwa huo unatibika.

Katika jamii, kuna baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumia muda mwingi kwenda kwa waganga wa kienyeji na watoto wao wakiamini kuwa wamerogwa na kuchangia tatizo kuzidi kukua siku hadi siku.

Wazazi na jamii wanamoishi watoto hao, wanawaona watoto hao ni tofauti na wengine kutokana na mienendo yao ya kila siku.

Mienendo hiyo ni pamoja na mtoto kuzunguka sehemu moja kila siku, kuzurura, kukimbiakimbia, kucheka cheka, kujing'ata na mingine mingi, vitendo ambavyo vinatafsiriwa na wazazi au jamii kuwa ni ugonjwa wa kurukwa akili au akili zake kuchukuliwa kwa imani za kishirikina.

Tuna kila sababu ya kulipongeza Shirika lisilo la faida la TAI Tanzania kwa kuibua tatizo hilo la Usonji nchini na kuanza jitihada za kutoa elimu katika jamii ili iweze kuwatambua watoto wanaokabiliwa na ugonjwa huo.

Tunaamini zaidi ya wanafunzi 2,000 wa shule za msingi jijini Dar es Salaam ambao TAI Tanzania imewafikia kwa kuwapatia elimu bora kwa kuwaonyesha picha ya katuni hiyo ya TIDI, kufanya majadiliano nao na kusikiliza mitazamo yao, watakuwa mabalozi wazuri kwenye maeneo wanayoishi na kuisadia jamii kuwaibua watoto wenye tatizo hilo.

Jihihada za TAI zisiishie hapo bali ziendelee kusambaza katuni hiyo FIDI inayoeleza hadithi ya mvulana mwenye Usonji, ikionyesha maisha yake ya kila siku, changamoto anazopitia na namna anavyokabiliana nazo kwa shule zote na kwenye mitandao ya kijamii ili wananchi wengi wapate elimu bora na kutokomeza ugonjwa huo nchini, kwani Tanzania bila Usonji inawezekana.

Tunaoimba serikali nayo iunge mkono jitihada ambazo Serikali ya Australia kupitia ubalozi wake nchini imeonyesha kukubali kuidhamini TAI Tanzania kwa kutoa fedha za kuendesha mradi wa kuibua watoto wenye tatizo hilo nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Vipaza sauti kuvuta wateja kero mpya

Na Mwandishi Wetu

**KERO** nyingine imeibuka nchini ya mtindo wa wafanyabiashara hasa wadogo maarufu kama Wamachinga kutumia vipaza sauti kutangaza biashara zao kwa lengo la kuvutia wateja, hivyo inapaswa kudhibitiwa kwa sababu imegeuka kuwa zogo na kusababisha kukosekana kwa maelewano na usikivu wa masikio.

Hata watu wanaokuwa katika maeneo hayo yenye kelele za vipaza sauti kwa muda mrefu wakiendesha shughuli zao, zikiwemo za mama lishe na baba lishe nao wamekuwa katika wakati mgumu wa kusikilizana na wateja kutokana na kelele hizo.

Watu wengine wanaokabiliwa na kero hiyo ni wale wanaohitaji msaada, huduma au ufanunuzi wa jambo fulani.

Katika vyombo vya habari kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa baadhi ya wananchi dhidi ya muziki kupigwa kwa sauti ya juu usiku kucha wakisema kuwa ni kero kubwa.

Wananchi hao wamekuwa wakilalamika kuwa kelele zinasababisha usumbufu kwao na kwa watoto wao nyakati za usiku na hadi wengine wakafika mbali kwa kuzifananisha na uharibifu wa mazingira.

Kelele hizo za muziki ambazo wananchi wamekuwa wakizililalamikia kwa muda mrefu kupitia vyombo vya habari zimekuwa zikitoka kwenye baa na klabu za usiku ambako biashara ya vileo hufanyika kwa lengo la kuwavutia na kuburudisha wateja wao.

Kwa mfano katika masoko mengi jijini Dar es Salaam, kila siku kuna wafanyabiashara wamekuwa wakiibuka na kutumia vipaza sauti kutangaza bidhaa wanazouza, matokeo yake badala ya kuwa kivutio, wamegeuka kero kwa wateja wao kutokana na maeneo wanayofanyia biashara kutawaliwa na zogo.

Vilevile kwenye mataa ya makutano ya barabara Bagamoyo na Sam Nujoma, kuna matangazo ambayo husikika tangu asubuhi

> **Kwa mfano katika masoko mengi jijini Dar es Salaam, kila siku kuna wafanyabiashara wamekuwa wakiibuka na kutumia vipaza sauti kutangaza bidhaa wanazouza, matokeo yake badala ya kuwa kivutio, wamegeuka kero kwa wateja wao kutokana na maeneo wanayofanyia biashara kutawaliwa na zogo.**

kwa kutumia kipaza sauti cha Soko la Machinga kuhamishiwa pale.

Mahali ambako spika hiyo imewekwa, kuna baadhi ya wafanyabiashara wanalalamika kuathiriwa na kelele za matangazo hayo kwa kukosa usikivu.

Wanadai matangazo hayo yamesababisha kuathirika kisaikolojia kutokana na kelele ambazo zinatoka kwenye spika ambayo imefungwa juu ya nguzo.

"Unavyoona ndio maisha yetu haya ya kila siku, muda mwingi tunautumia hapa tangu asubuhi hadi saa 4 usiku kelele hizo hizo za soko la Machinga limehamia hapa wateja karibuni... hatuna jinsi tunavumilia watoto lazima wale," anasema mmoja wa wafanyabiashara hao.

Serikali inapaswa kuingilia kati kwa kuchukua hatua kudhibiti kelele hizo kwani pamoja na kuwa kero zinaathari kisaikolojia, usikivu wa masikio na afya ya akili.

Mara kwa mara Serikali imekuwa ikipiga marufuku kelele kwenye baa na kumbi za sterehe na si biashara za vileo kwa kuwa zimekuwa zikitoa ajira huku yenyewe ikikusanya mapato.

Vivyo hivyo, ifanye kwa wafanyabiashara hao kwa kuendesha biashara zao pasipo kutumia vipaza sauti na kuyafanya mazingira yao kuwa salama na tulivu wakati wote.

Serikali kupitia Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) inatakiwa kuingilia kati kwa kudhibiti tabia hiyo kwa sababu imeendelea kusambaa hadi kwenye vituo vya daladala kwa madereva wa bodaboda na bajaj kufunga vipasauti vikitangaza safari zao ili kuvutia abiria.

Ikumbukwe kuwa katika masoko na maeneo ambako vipaza sauti vimekuwa vikitumika kuvutia wateja na abiria, kuna barabara kubwa zinapita, hivyo inakuwa vigumu mlio wa gari kusikika, jambo ambalo linaweza kusababisha watu kupata ajali kwa kugongwa na vyombo vya usafiri.

HABARI KITAIFA

# TIC kufanyia kazi utitiri wa tozo kwa wawekezaji

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimeahidi kufanyia kazi kilio cha wawekezaji kuhusu utitiri wa tozo wanazotozwa na taasisi mbalimbali za serikali.

Ahadi hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya TIC, Dk. Binilith Mahenge, alipotembelea viwanda mbalimbali Dar es Salaam na kuelezwa na wafanyabiashara hao kuhusu utitiri wa tozo hizo.

Kilio cha wafanyabiashara hao ni tozo wanazotozwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Wakala wa Usalama na Afya Pahali pa Kazi (OSHA), Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Wakala wa Vipimo (WMA).

Dk. Mahenge alisema baada ya ziara yake, ataitisha kikao na kufanya tathmini kuangalia kama kuna umuhimu wa taasisi zote hizo za serikali kuwatoza tozo wafanyabiashara na wenye viwanda.

Pia alisema amesikia kilio chao kuhusu tatizo la masoko na kuahidi kuwa TIC itawaunganisha na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade) ili wayafikie masoko ya kimataifa.

"Tutahakikisha mnakuwa karibu sana na TANTRADE (mamlaka ya Maendeleo ya Biashara) kwani wao wanajua masoko yaliko na mfanye utafiti kuonyesha kwamba bidhaa zenu zinashindwa kushindana kwenye masoko ya nje kwa sababu bidhaa za wenzenu zinasamehewa kodi.

"Mfano muwe na takwimu kwamba tumelinganisha bidhaa yetu na ya Kenya, Uganda au Zambia tumeona wenzetu bei ni ya chini kulinganisha na zetu na mkiweza kufanya hivyo itakuwa rahisi kwa serikali kujua namna ya kuwasaidia," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda cha AKBERALIS Hardware and Electric, Hussein Alibhai, alisema maofisa wa serikali wanafanya jambo jema kufuatilia maendeleo ya biashara za wawekezaji ikiwemo kufanya ukaguzi lakini tatizo majukumu ya taasisi nyingi yamekuwa yakifanana.

"Mfano anaweza kuja mtu wa NEMC na OSHA, ambao ukiangalia majukumu yao kama yanalingana kwa hiyo inakuwa usumbufu kwa mwekezaji tunashauri wawe wanaangalia kero ambazo wafanyabiashara wanakabiliana nazo," alisema.

Aliiomba serikali isikilize kilio chao kwani isipofanya hivyo baadhi ya wawekezaji wanaweza kuogopa kuja kuwekeza nchini kwa kuhofia usumbufu wa taasisi hizo.

"Tunaomba kwa dhati kabisa serikali ipunguze hizi taasisi zinazokuja kuchukua tozo kwetu maana zimekuwa changamoto kubwa sana kwetu.

Hatukatai kufanyiwa ukaguzi lakini tozo zimekuwa mzigo mkubwa sana kwetu wawekezaji," alisema.

Alisema kiwanda chao bado ni kidogo na kinahitaji kukua kwa kuwa na teknolojia ya kisasa ya kuzalisha mali nyingi hivyo kuongeza kiwango cha ajira kwa vijana.

"Serikali itusaidie kukua tupate teknolojia ya kisasa ambayo itatuwezesha kuuza zaidi na kuchangia kiasi kikubwa kwenye ukuaji wa pato la taifa lakini tukiendelea na hali hii itachukua muda kwetu kukua," alisema.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia) akimwapisha Aziza Ally kuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM) mkoa wa Tabora, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wabunge walia upungufu watumishi afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wameiangukia serikali kutatua upungufu wa watumishi wa kada ya afya.

Wakiuliza maswali bungeni jana, Mbunge wa Viti maalum (CCM), Catherine Magige, alihoji lini serikali itamaliza tatizo la watumishi wa kada ya afya katika vituo vya afya Karatu Mjini na Kaloleni

"Kituo cha Kaloleni kinahudumia wananchi wengi wa Jiji la Arusha na kuna watumishi saba ambao wamefanya kazi kwa muda mrefu bila mkataba. Je, serikali haioni ni wakati sasa wa kuwapa ajira ya kudumu?" alihoji.

Alisema mtaani kuna watumishi wengi wa kada ya afya wanaosubiri ajira serikalini na binafsi, hivyo kuhoji serikali haioni umuhimu wa kuwatumia watumishi hao wafanye kazi kwa kujitolea ili kuziba pengo la upungufu uliopo na baadaye wapewe ajira rasmi.

Naye, Mbunge wa Itilima (CCM), Njalu Silanga, alisema zaidi ya zahanati 10 katika wilaya ya Itilima zimepata kibali lakini hazina watumishi wa kada hiyo na kuhoji kauli ya serikali.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Munde Tambwe, alisema kuna upungufu wa watumishi hao kwenye zahanati za pembezoni mkoani Tabora na kuhoji lini serikali itapeleka watumishi wa kutosha.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk. Festo Dugange, alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 na 2022/23 serikali imeajiri na kuwapangia vituo watumishi 83 wa kada mbalimbali za afya katika halmashauri ya Wilaya ya Karatu, na watumishi 79 katika Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Pia alisema watumishi 14 walipangwa katika kituo cha afya Karatu Mjini na watumishi 18 katika kituo cha afya Kaloleni jijini Arusha.

"Serikali itaendelea kuajiri wataalam wa kada mbalimbali za afya na kuwapanga katika vituo vyenye upungufu mkubwa kote nchini, zikiwamo halmashauri za Karatu na Arusha Jiji," alisema.

Dk. Dugange alisema serikali imeweka utaratibu mzuri wa kutoa kipaumbele cha ajira kwa watumishi ambao wanajitolea.

"Tutaangalia vigezo vyao ndani ya kipaumbele cha kuajiri ili wapate ajira za kudumu, tayari serikali ilishatoa mwongozo wa wahitimu wote wa kada ya afya kuomba kujitolea kwenye vituo vya afya na wakurugenzi wenye mapato wawaajiri kwa mikataba," alisema.

Kuhusu Itilima, Naibu Waziri huyo alisema Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ni miongoni mwa Halmashauri zenye upungufu mkubwa wa watumishi na Rais Samia Suluhu Hassan katika ajira za watumishi wa kada hiyo ametoa kipaumbele katika Halmashauri na Mikoa yenye upungufu mkubwa zaidi ikiwamo Mkoa wa Simiyu.

"Katika miaka hii mitatu ya Rais ameajiri watumishi wengi wa kada ya afya na mara ajira zitakazojitokeza watumishi watapelekwa kwenye vituo vyenye upungufu mkubwa ikiwamo Tabora,"alisema.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Profesa Mwandosya ataka sera matumizi akili bandia

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa zamani wa katika serikali ya awamu ya tatu na ya nne, Profesa Mark Mwandosya, ameishauri serikali kutunga sera ya kudhibiti matumizi ya akili bandia ili kuzuia watu kutumia vibaya teknolojia hiyo.

Alitoa ushauri huo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mjadala ulioandaliwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na kufanyika chuoni hapo.

Profesa Mwandosya ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Ofisi ya makamu wa Rais (Mazingira), Maji na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Kazi maalum), alisema bila kuwapo udhibiti wa teknolojia hiyo, wanaweza kuibuka watu wakaitumia vibaya na kusababisha taharuki kwenye jamii kwa kufanya mambo ambayo hayapendezi.

Alisema teknolojia duniani inaendelea kukua kwa kasi tofauti na matarajio ya watu wengi na baadhi ya nchi wanatumia teknolojia hiyo kutengeneza vifaa kama kompyuta na magari.

"Ukiangalia kwenye viwanda vingi kwenye nchi zilizoendelea kwa sasa mashine ndizo zinafanyakazi ambazo awali zilikuwa zinafanywa na binadamu na zinafanyakazi hizo kwa haraka na kwa ubora zaidi bila matatizo," alisema.

"Tusipoangalia watu ambao hawawatakii mema binadamu wengine wanaweza kuitumia hiyo tekbolojia vibaya kwa hiyo naona umefika wakati wa kuwa na sera ya kudhibiti kwa sababu uzoefu unaonyesha kwamba biashara inapenda sana kushamiri ambako hakuna sera wala udhibiti, " alisisitiza.

Prof. Mwandosya ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA), alisema hivi sasa dunia inaondokana na magari yanayotumia mafuta ambayo yamekuwa yakizalisha hewa ya ukaa inayosababisha joto duniani.

Alisema wazalishaji wa magari wanaondokana na teknolojia ya magari ya sasa yanayotumia petrol na dizeli na kwenda kwenye matumizi ya betri za umeme na wameshaanza kuyatengeneza.

"Bila shaka nasisi Tanzania tutakuwa tumeliona hilo kwa hiyo kwa upande wetu tunapaswa kuanza kutengeneza sera ya matumizi ya magari ya umeme, nimesisitiza hilo kwa sababu Tanzania tumegundua madini ambayo yatatengeneza betri zinazotumika kwenye magari ya umeme," alisema

Alisema kuna nchi duniani zimegundua teknolojia ambapo mtu anaweza kuchaji betri kwa dakika kumi na kusafiri na gari lake kutoka jijini Dar es Salaam hadi mkoani Mbeya bila kulazimika kuchaji tena.

"Lazima tufanye kitu tusingoje teknolojia itukute wakati hatujajitayarisha tunaweza kuwa kwenye matatizo kwa hiyo lazima wataalamu tuishauri serikali kuja na sera itakayolisaidia taifa tusije kujikuta tunaishi kwenye karne iliyopita," alisema

Mkurugenzi wa Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Dk. Nkundwe Mwasaga, alisema teknolojia inatakiwa kuongeza ubunifu na kuchochea shughuli mbalimbali za kiuchumi.

"Sisi tume tunasimamia masuala ya mapinduzi ya kidijitali na kwenye mapinduzi hayo tunaangalia nguzo tano, moja ya nguzo hizo ni kuongeza ujuzi wa watanzania, kuhakikisha mifumo inakuwa salama na inawezakuaminina, kuhakikisha huduma za mawasiliano zinapatikana maeneo yote bila ubaguzi wowote, kutengeneza uchumi wa kidijitali unaojumuisha watanzania wote na kuhakikisha masuala ya utafii ubunifu na ujasiriamali wa kidijitali unatumiwa vizuri ili tuwe na kampuni nyingi za kisasa," alisema.



Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Tanga, Omari Ayubu (wa pili kushoto), akikagua ujenzi wa daraja jipya katika Mto Amtico, kata ya Genge Kwamtiga, akiwa ziara yake ya siku mbili ya kukagua miradi ya maendeleo wilayani Muheza jana. Wa (sita kushoto) ni Katibu Tawala wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wawili wafariki ajali magari manne

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU wawili ambao bado hawajafahamika majina yao, wamefariki dunia na wengine wanane kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha magari manne eneo la Ichunilo, Mto Ruhuji katika Mlima wa Kibena barabara kuu ya Njombe - Ruvuma.

Ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 3:00 asubuhi mjini hapa.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Njombe (Kibena), Dk. Helen Msese, alithibitisha vifo vya watu wawili ambao bado hawajafahamika majina yao huku akibainisha majeruhi wanane wanaendelea na matibabu katika hospitali hiyo.

"Tumepokea majeruhi wanane kati yao wanawake ni wawili na wanaume sita na waliofariki ni wawili ambao ni wanaume. Kwahiyo jumla tumepokea watu 10 na kati ya hao, majeruhi wawili hali zao si nzuri, mmoja ameshaanza kufanyiwa upasuaji na mmoja tumempa rufani kwenda hospitali ya (rufani ya mkoa," alisema Dk. Msese.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji Mkoa wa Njombe, Bahati Mkutani, alisema baada ya kupokea taarifa walifika eneo la tukio kwa ajili ya ukoaji.

Alisema katika eneo hilo, awali walikuwa wakifanya uokoaji kwenye lori la kwanza lililoanguka likiwa limebeba saruji na baadaye lori lingine lililobeba mchanga likafeli mfumo wa breki na kuparamia magari takribani manne pamoja na watu waliokuwa katika eneo hilo la uokoaji.

"Leo (juzi) asubuhi majira ya saa 3:00 asubuhi, tulipokea taarifa kuwa kuna ajali eneo la Ichunilo. Tukiwa tunaendelea na uokozi ikatokea ajali nyingine ya pili hapa hapa," alisema Mkutani.

Mmoja wa mashuhuda wa ajali hiyo, Geofrey Kaberege, alisema walikuwa wanatoka Lupembe na walipofika katika mteremko wa Kibena, walizuiwa kwa sababu ya ajali.

"Mara ghafla kwa nyuma kukatokea lori lilikuwa limepoteza mwelekeo. Kwa jinsi nilivyoliona lilifeli breki likawa linagonga nyuma ya gari na mbele lilivyomaliza, mbele kulikuwa na magari ambayo yalikua yanatoa msaada nayo yakagongwa,"alisema Kaberege.

## Balozi aonya unyanyapaa kwa wenye usonji

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Australia nchini, Luke Willliams, amesema watoto wenye ugonjwa wa usonji wanakumbwa na unyanyapaa na unyanyasaji katika jamii duniani kote.

Balozi Willliams aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa katuni inayoelezea jinsi ya kuwatambua watoto na vijana wenye usonji na jinsi ya kukabiliana na vitendo hivyo katika jamii.

Alisema watoto wenye usonji nchini na duniani wanakumbana na vitendo hivyo na kuwa katuni hizo zitakuwa hatua bora ya kutoa elimu ya jinsi ya kuwatambua vijana na watoto wenye ugonjwa huo katika na jamii.

Awali, Mkuu wa Programu na Uendeshaji wa Shirika lisilo la faida la TAI Tanzania, Debora Maboya, alisema zaidi ya wanafunzi 2,000 wa shule za msingi jijini Dar es Salaam wamekwisha kuangalia katuni hiyo, kufanya majadiliano nao na kutoa mitazamo yao.

Debora, alisema baada ya uzinduzi, TAI inatarajia kusambaza katuni hizo kwa shule zote nchini na kwenye mitandao ya kijamii katika kipindi cha miezi ijayo kwa udhamini wa ubalozi huo nchini.

Alisema lengo ni kusambaza elimu ya ugonjwa huo kwa wananchi wengi zaidi ili wajue namna ya kuwatambua watoto na vijana wenye usonji na kuachana na vitendo vya unyanyasaji na unyanyapaa dhidi yao.

TAI Tanzania imetengeneza katuni hiyo mpya iitwayo FIDI kwa kushirikiana na Kituo cha Kutibu Watoto cha Gabriella Rehabilitation Center kwa kutumia watu hai wenye usonji, familia zao na marafiki kwa udhamini wa ubalozi huo nchini.

FIDI inaeleza hadithi ya mvulana mwenye usonji ikionyesha maisha yake ya kila siku, changamoto anazopitia na namna anavyozikabili.

TAI limeandaa katuni hiyo kwa ajili ya kuleta mabadiliko ya kijamii na kitabia kwa kutumia mtindo wa 3D, maigizo ya redio na vijarida vya katuni ili kufikisha ujumbe katika jamii hususani vijana wa rika dogo nchini.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), mtoto mmoja kati ya watoto 100 wanasumbuliwa na usonji na inakadariwa kuwa asilimia 1.2 ya Watanzania wamegundulika kusumbuliwa na ugonjwa huo.

Inaelezwa kuwa kumekuwa na unyanyasaji na unyanyapaa kwa waliopimwa na kugundulika kuwa na ugonjwa huo ambao dalili zake ni pamoja na mtoto kuzunguka sehemu moja, kutembelea na kung'ata kung'ata.

Mmoja wa wakazi wa Dar es Salaam, Josephine Sanga, alisema mtoto wake akiwa na miezi kumi baada ya kujifungua alikumbwa na ugonjwa wa degedege.

Alisema baada ya kumpeleka hospitali na madaktari kumfanyia uchunguzi, walibaini kuwa ana usonji. "Waligundua kuwa nilijifungua mtoto wangu akiwa na usonji, degedege ilikuwa ni sababu tu," alisema Josephine.

Alisema mwanawe ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 14, anaendelea vizuri kwa kuwa anaweza kufanya baadhi ya shughuli, ikiwamo kulima bustani ya mboga. "Namshukuru Mungu kwa hatua ambao mwanangu amefikia, si rahisi kuwa na maendeleo hayo kama ambavyo nimeshuhudia kwa watoto wengine wa ugonjwa kama huu wa mwanangu," alisema.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mtakuja Beach, jijini Dar es Salaam, Aman Duma, alisema wamekuwa kama sehemu ya jamii kuelimisha wanafunzi kuhusu usonji kwa kuwa watakuwa ni mabalozi wa kwenda kusambaza elimu hiyo kwa watu wengi zaidi na kuwatambua watoto na vijana wenye ugonjwa huo.


Polisi Kata ya Magila, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Inspekta Frank Mwemsi akitoa elimu ya usalama barabarani na ulinzi shirikishi kwa vijana waendesha pikipiki za kubeba abiria maarufu bodaboda katika kijiji cha Mikwamba, juzi.
**PICHA: STEVEN WILLIAM**

# TAKUKURU yarejeshea wanafunzi michango bima afya waliyokatwa

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imerejesha kwa wanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii kilichoko Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Sh. 626,000 za michango ya bima, ambayo walikatwa kwa ajili ya kugharamia huduma hiyo, ambazo hazikutumika.

Kurejeshwa kwa fedha hizo, kumetokana na uchunguzi uliofanywa katika mfumo wa matumizi ya fedha na taasisi hiyo.

Mkuu wa TAKUKURU, Mkoa wa Kilimanjaro, Frida Wikesi, alisema katika mwaka wa fedha 2023/24, uchunguzi wao katika mfumo huo umebaini kuwa fedha hizo za bima ya afya zilikuwa zikipokelewa mkononi, hazitumiki kutoa huduma iliyokusudiwa na hazikupelekwa benki.

Taarifa ya Wikesi, inatokana na utekelezaji wa majukumu yake katika robo ya Julai hadi Septemba 2023.

Kuhusu hatua iliyochukuliwa, Wikesi, alisema elimu imetolewa kwa wanachuo hao na wakufunzi wao kuhusu haki hiyo na namna wanapaswa kuziingiza katika mfumo.

"Baadhi ya wanachuo wamerejeshewa fedha za bima kwa ambao hawakupata huduma hiyo. Hata hivyo, makosa ya jinai uchunguzi umeanza," alisema.

Kuhusu mradi wa ujenzi wa bwalo la Shule ya Sekondari Kibacha, wenye thamani ya Sh. milioni 100, ni pamoja na mafundi/wakandarasi wake hawana mikataba, taratibu za kuwapata hazijulikani na sheria za ununuzi zimevunjwa.

Aidha, makosa kama hayo yamo pia katika mradi wa ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Kisima, wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 584.28.

# Madiwani wahoji kukatwa bima afya bila huduma

**Na Mary Mosha,** ROMBO

GHARAMA kubwa za matibabu na kushindwa kufikia baadhi ya huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali, zimewaamsha madiwani wa Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro, kulilia mchakato wa kuwapatia kadi za bima ya matibabu.

Madiwani hao wamelalamikia utaratibu wa kujigharamia malipo ya huduma za afya, wakati tayari walishakatwa fedha za kugharamia huduma hiyo zaidi ya miezi mitatu.

Kilio cha madiwani hao kilisikika juzi kwa mara ya kwanza katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichoketi kujadili na kupitisha taarifa ya mapato ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24.

Diwani wa Athuman Kimaro, alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya hiyo, kuangalia upya suala la bima za afya kwa madiwani, kwa kile alichodai kukatwa posho zao bila kupata huduma hiyo wanapofika katika vituo vya afya.

"Tunapata shida tunapofika hospitalini, juzi nimeenda hospitali kupatiwa matibabu, nilipofika naambiwa bima yangu haifanyi kazi. Huu ni udhalilishaji, tunaiomba serikali ichukue hatua ili tuweze kupata haki zetu, kwa kuwa tunakatwa kwenye posho zetu," alisema.

Diwani Venance Malleli alisema: "Nimekuwa nikikatwa fedha ya bima bila kutaka na sijawahi kuomba, licha ya kulazimishwa na bado bima hizo hazifanyi kazi. Naomba serikali ione kama kuna uwezekano tutolewe kwenye mpango huo."

Akisisitiza malalamiko hayo, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Gilbert Tarimo, alisema baada ya kushughulikia kadi hizo katika hatua mbalimbali, wapo baadhi ya madiwani bima zao zimeanza kufanya kazi.

"Tuna diwani mgonjwa, tulikuwa tunashughulikia upatikanaji wa bima yake, na leo (jana), ametujulilisha bima hiyo imeanza kufanya kazi. Madiwani wengine tizameni bima zenu tena kama zimeanza kufanya kazi. Lakini tuendelee kuiomba serikali, kuharakisha huduma hii kwa madiwani," alisema Tarimo.

Akijibu hoja hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Godwin Chacha, aliwataka madiwani hao kuwa wavumilivu, wakati serikali ikiendelea kushughulikia suala hilo.

"Tukumbuke kuwa posho hizi ziliondolewa halmashauri na kupelekwa TAMISEMI (Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), na sisi tumeshaandika barua na kupitisha kwa viongozi wetu wa mkoa ili kuona namna ya kutatua tatizo hili.

...Hii sio hapa kwetu tu ni Tanzania mzima. Niwaombe muwe wavumilivu, adha hiyo itafika mwisho," alifafanua Chacha.

# CCBRT Moshi yaomba serikali utaratibu uchangiaji huduma

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KITUO cha Huduma za Utengamao kwa Watu Wenye Ulemavu cha CCBRT- Moshi, kimeiomba serikali kufikiria jinsi ya kuanza kuchangia gharama za uendeshaji wa kituo hicho pamoja na mishahara kwa watoa huduma, baada ya wafadhili wake wa nje, kupunguza ufadhili kwa zaidi ya asilimia 90.

Meneja wa Kituo hicho, Lucy Kavishe, alisema kwa sasa ufadhili huo umepungua kwa kiasi kikubwa na kwa muda mrefu, jambo ambalo limewalazimisha kupunguza na kwingine kusitisha kabisa baadhi ya huduma wanazozitoa kwa watu wanaowahudumia, pamoja na watoa huduma wao.

"Shughuli za kituo hiki kwa zaidi ya asilimia 90 zinategemea ufadhili kutoka nje. Ni matumaini yetu ombi letu litapatiwa ufumbuzi ili tuweze kuendelea na huduma kwa Watanzania wenzetu," alisema Kavishe.

Matatizo mengine yanayokikabili kituo hicho kwa sasa, ni gharama kubwa na upatikanaji wa shida wa vifaa tiba, kwa watu wenye ulemavu na hali duni ya kiuchumi miongoni mwa familia za watoto wenye ulemavu, ambayo husababisha watoto hao kushindwa kupata huduma stahiki na kwa wakati.

Nyingine ni miundombinu katika majengo kama ofisi za umma, shule, hospitali na katika vyombo vya usafiri, bado siyo rafiki na ni tatizo hasa kwa watumiaji wa vifaa saidizi kama viti mwendo.


Aidha, tatizo jingine ni uchakavu wa magari ya kutoa huduma na uchache wa wataalamu wanaotoa huduma ya utengamao.

Kwa mujibu wa Kavishe, pamoja na huduma za utengemao zinazotolewa kituoni hapo, huduma za mkoba pia zinatolewa katika jamii ya Mkoa wa Kilimanjaro, pia wanashirikiana na wadau mbalimbali kutoa huduma katika Mikoa ya Arusha,

Manyara, Singida, Tanga, Dodoma, Iringa, Shinyanga, Kigoma na Morogoro. Alisema kwa zaidi ya miaka 25, kupitia kituo hicho cha CCBRT-Moshi, maarufu kama 'nyumba ya matumaini' wametoa huduma kwa watu wenye ulemavu na familia zao, zaidi ya 18,000.

CCBRT-Moshi, hutoa huduma ya kliniki ya vifaa tiba, mafunzo juu ya lishe, na baada ya wiki maalumu ya mazoezi, watoa huduma majumbani na wataalamu, humfuatilia mteja kwenye jamii na kuwapatia mafunzo mbalimbali, ikiwemo jinsi ya kujikwamua kiuchumi, matumizi sahihi ya vifaa na, uangalizi wa vifaa vyao saidizi.

Huduma nyingine zinazotolewa na kituo hicho, ni huduma kwa watoto wachanga waliozaliwa na miguu kifundo, kliniki ya wateja wa kutwa, kliniki ya viti mwendo/vifaa tiba, ambavyo wahitaji hutengenezewa vifaa hivyo kulingana na uhitaji wao. Mfiziotherapia wa Kituo cha CCBRT-Moshi, Sabas Kimario, akizungumzia huduma hizo, alisema mpaka sasa kuna vituo 30 vya kutoa huduma hiyo katika vituo vya afya na zahanati katika Wilaya ya Moshi.





## Vijiji 21 kumegwa hifadhi ya msitu

**Na Halima Ikunji,** KALIUA

VIJIJI 21 vilivyoko ndani ya hifadhi ya msitu wa Mto Igombe, Ulyankulu mkoani Tabora, vinatarajiwa kumegwa na wakazi wake kupelekwa katika eneo litakalopangwa na serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Rashid Chuachua, alisema hayo jana katika mkutano wa hadhara ulioviku-tanisha vijiji vitano vya Nhwande, Ntigu, Imagi, Nsungwa na Ibapa na kwamba watakabidhiwa maeneo yaliyopimwa tayari pamoja na hati.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wanaishi katika maeneo ya kudumu na kuondoa adha za kuhamahama, hivyo wakishahamishwa katika vijiji vyao, watapewa hati halali za umiliki wa ardhi bila malipo.

Chuachua pia alisema tayari serikali imetoa maelekezo kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuweka mipaka kwenye vijiji vyote ambavyo vinahesabika kuwa hifadhini ili viondolewe.

"Serikali imemega eneo katika hifadhi hii ya msitu wa Mto Igombe ambalo wakazi wa vijiji hivi watapewa kwa ajili ya kuendelea na shughuli zao. Baada ya TFS kuweka mipaka, wananchi waliopo ndani ya hifadhi wataondolewa na kupatiwa maeneo yaliyopimwa," alisema.

Katibu wa CCM Wilaya ya Kaliua, Eliud Shemawia, aliwataka wananchi watoke kwenye maeneo ya hifadhi na warudi kwenye eneo salama ili waepushe ugomvi na serikali.

Alisema serikali iwape wananchi maeneo makubwa ili waendeshe shughuli zao za kilimo na ujenzi, kama kutakuwa na uhitaji kutakuwa na maombi mengine kwa baadaye.

# Mwongozo kuwezesha halmashauri wa kuondokana na utegemezi waiva

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji (UNCDF) kwa kushirikiana na serikali limeanzisha mwongozo wa uanzishwaji na usimamizi wa kampuni mahsusi za uendeshaji wa miradi ya vitegauchumi kwenye mamlaka ya serikali za mitaa.

Mwongozo huo utazisaidia halmashauri kujitegemea katika usimamizi na utekelezaji miradi ya vitegauchumi.

Katika hatua za awali za utekelezaji wa mwongozo huo, UNCDF na serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa, zimeanzisha mafunzo maalum kwa wataalam mbalimbali ngazi ya taifa kuhusu matumizi ya mfumo huo watakaotoa elimu katika ngazi za halmashauri.

Lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha mwongozo huo unawafikia wataalam katika ngazi za mitaa na kuziwezesha halmashauli kuongeza kiwango cha mapato ili kuzisaidia katika utekelezaji na usambazaji wa huduma za jamii.

Akifungua mafunzo hayo juzi, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Balandya Elikana, alisema pamoja na sera, sheria na miongozo mbalimbali, bado mamlaka za serikali za mitaa zinakabiliwa na changamoto katika usimamizi wa miradi ya kiuchumi ikiwamo kuingiliwa kisiasa na uzoefu mdogo wa watendaji.

Alisema mwongozo huo utaziwezesha mamlaka ya serikali za mitaa kuandaa maandiko ya miradi inayokidhi mahitaji ya kupata fedha mbadala kutoka kwenye vyanzo vingine zikiwamo taasisi mbalimbali za kifedha kama benki na kuuza hati fungani.

Ofisa Uwekezaji kutoka UNCDF, Stella Lyatuu, alisema mwongozo huo tayari umesha andaliwa na kupata baraka za serikali na wameanza kutoa mafunzo kwa wataalamu ngazi ya taifa ambao watatoa mafunzo hayo katika ngazi za halmashauri ambao ndio watumiaji wakuu.

"Huu mwongozo utawasaidia kujua namna ya kuendesha miradi kiufanisi ili kutekelezwa kitaalamu wapate kufikia malengo yale yaliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kuondokana na utegemezi katika serikali kuu na kuwahudumia wananchi kwa wakati,"alisema.

Mkurugenzi Msaidizi Uratibu Shughuli za Serikali kwenye Mikoa TAMISEMI, Johnson Nyingi, alisema awali ugharamiaji mkubwa wa miradi ya serikali za mitaa ulikuwa ukitegemea serikali kuu, hivyo serikali imelenga kuziwezesha halmashauri kujitegemea kwa asilimia kubwa katika kuwahudumia wananchi na kukusanya mapato.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Balandya Elikana akifungua mafunzo maalumu kwa wataalamu mbalimbali ngazi ya taifa kuhusu matumizi ya muongozo wa uanzishwaji na usimamizi wa kampuni mahususi za uendeshaji wa miradi ya vitega uchumi kwenye mamlaka ya serikali za mitaa (SPV), jijini Mwanza jana. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Waliopisha ujenzi stendi kulipwa fidia

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, amemwagiza Mkurugezi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, kufanya tathimini na kulipa fidia haraka kwa wananchi 29 waliopisha ujenzi wa stendi inayoendelea kutumika kwa zaidi ya miaka 10 sasa.

Wananchi hao wanadai kuondolewa katika eneo hilo kupisha ujenzi wa stendi hiyo mwaka 2010 lakini mpaka sasa wamekuwa wakizungushwa na halmashauri bila kulipwa fidia yao ya zaidi ya Sh. milioni 308 huku wakizuiwa kufanya shughuli zao za maendeleo.

Kilio cha muda mrefu cha wananchi hao kiliibuka juzi katika mkutano na mkuu wa mkoa wakati akisikiliza na kutatua kero za wananchi wilayani hapa.

Kwa mujibu wa wananchi hao, licha ya stendi hiyo kuendelea kufanya kazi, hakuna fedha waliyolipwa na wamekuwa wakifuatilia malipo na kuishia kuambiwa kuwa suala lao linafanyiwa kazi.

Baada ya kusikiliza kilio hicho, Makalla alimtaka mkurugezi, mkuu wa wilaya na ofisa ardhi kufika eneo la stendi ili kujiridhisha kisha kamati ya fedha ikae ili kuwalipa fidia zao haraka.

Mkurugezi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Binuru Shekidele, alisema awali walilipa fidia wakajua wamemaliza lakini kuna watu walijitokeza tena wakidai fidia ndipo wakaamua kufanya tathimini tena Agosti 10, mwaka huu, kwa watu 29.

Alisema, katika tathimini hiyo walibaini kuwa watu hao 29 wanaidai kalmashauri Sh. milion 308 ambazo zinatakiwa kulipwa kama fidia.

Ofisa Ardhi wa Halmashauri hiyo, Seth Lyanga, alikiri kuwapo kwa wananchi ambao bado hawajafidiwa na wanadai tangu mwaka 2010 lakini wanaendelea kuwalipa kwa awamu na wamebaki watu 29 ambao ndio waliowasilisha kero yao.



Ukurasa 13

Tuangalie wasanii aina hii wasitupeleke gizani


# BUFE

IJUMAA NOVEMBA 10, 2023

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe




## KUTOKA TANI 122 HADI 370...

## Brazil inavyoisaidia Tanzania kupiga hatua na mradi pamba, Tabora yavutiwa iwe mtaji wake

Ukurasa 12

## UTAWALA BORA & THAMANI YA NAULI...

# RC Chalamila alivyopiga saluti kwa Rais kwenye reli ya Gongolamboto

**Na Peter Orwa**

HADITHI ya Dar e Salaam sasa, ni mkasa wa abiria wa treni ya daladala inayofanya kazi kati ya Pugu na Kariakoo Gerezani, wamejaa hadi kwenye kichwa cha safari.

Hapo ikamkera hasa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, mahali aliko na akamnyayulia simu mwakilishi wake Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, akimhoji majibu ya kinachojiri kiusalama.

Mara moja mkuu huyo wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kimawazo akavaa buti na magwanda, akipiga saluti kwa kuongozwa na usemi na kijeshi "the quest of command is the commanding question" ikiimaanisha anachohoji au kuomba kamanda ni amri, ikizingatiwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ni yeye Rais.

Hapo akaingia kazini na kamati yake kimkoa Jumanne hiyo, pia wadau wakuu Shirika la Reli Tanzania (TRC), Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Polisi, hata wasimamizi wa Barabara LATRA, huku mwenyewe kama kamanda mpokea amri akiongeza medani binafsi kupata majibu ya ziada na suluhisho.

Jumanne asubuhi, mara moja akiwa na timu iliyokamilika kukabili kashfa hiyo ya kimkoa, akatinga na treni kusafiri kati ya Pugu na Gerezani.

Akiwa ameshapata dondoo za kisa na mkasa watu kunadi treni kutoka kwa wahusika na medani zake, Chalamila akatumia saa 24 kufikia hatua hiyo. Katika moja ya majumuisho ya awali, baada ya kuupa maagizo ya 'kikao sasa hivi' na kuwakosoa, ikawa dozi muhimu katika uendeshaji taasisi TRC kwa mfumo wa sasa.



Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila, akiwa stesheni Dar es Salaam, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

"Enyi msiwe kama TRC ya enzi zile jamani..." akatamka Chalamila kwa sura ya kukereka. Kimsingi, ni nukuu muhimu kwa shirika hilo, ingawa Chalamila kaitoa katika mchanganyiko wa ukali na masihara.

Msingi wake ndicho anachosisitiza Rais Dk. Samia sasa na ndicho kilihimizwa sana katika mabadiliko ya mpito wa kutoka mfumo hodhi kwenda huria mwaka 1985.

Wakati asasi kama Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani (IMF) zikiwekeza mikakati mbalimbali nchini wakati huo kusaidiana na serikali, kama vile Mpango wa Marekebisho ya Uchumi (ERP), katika hatua mbalimbali.

Ndani yake kuna mawili yalihimizwa katika uendeshaji uchumi na biashara kitaifa; Utawala Bora, kuhakikisha haki na Ufanisi wa Uendeshaji Uchumi serikalini. Hapo ndipo ikawa chimbuko la mwaka 1995, kuzaliwa Wizara ya Rais Utawala Bora.

Mifumo ya Utawala Bora ina uwiano wa serikali, mahakama na bunge, huku umaarufu wa vyombo vya habari ukimea kama nguzo ya nne isiyo rasmi, ikiwamo kuzaliwa vyombo vya habari vya IPP.

Kwenye mfumo wa ufanisi nchini, kukahimizwa nadharia mpya 'thamani ya fedha' maarufu 'value for money', kwa maana huduma ifanane na thamani inavyogharimiwa, huku mteja akipata hadhi ya ufalme anakohudumiwa, ndio uhalisi wa uchumi huria na wenye ushindani.

Ni zama kukashudiwa miradi mingi ya kimataifa yenye sura ya mikopo, ikawa na wasimamizi wakiwa na magari yenye usajili wa 'DFP' huku dhana hiyo ikiingizwa katika mitaala ya uchumi kuanzia shule hadi vyuoni, ijengeke kwa umma.

Ni ndani ya nadharia hiyo, dhana hiyo ikajitokeza bungeni sasa, chombo cha mwendokasi Dar es Salaam kiwekewe mshindani, huku kukishuhudiwa Rais Dk. Samia anaamua kubinafsisha huduma za Bandari Dar es Salaam, kusaka ufanisi.

Ni kupitia nguzo ya nne ya dola, gazeti Nipashe ndilo lililoibua kinachojiri katika ufanisi wa treni ya daladala watu kudandia, Jumanne wiki hii.

Hapo ndio inapokuja jibu la majumuisho ya agizo la Mkuu wa Mkoa Chalamila, akitekeleza maelekezo ya Rais akitamka "...enyi (menejimenti) msiwe kama TRC ya wakati ule..."

Mvuto wa mageuzi ya Chalamila, yameenda mbali kutafsiri utawala bora kwanza kwa 'kupigia saluti' agizo la rais ndani ya muda mfupi, kisha akajua siri ya madhila hayo na kuhamia kwenye majibu.

Ni dhana ambayo imekuwa na maana kubwa katika biashara ya

Inaendelea Uk 14

## BIASHARA

KUTOKA TANI 122 HADI 370…

# Brazil inavyoisaidia Tanzania kupiga hatua na mradi pamba, Tabora yavutiwa iwe mtaji wake

• Wakulima laki tano, ekari milioni, waingiza Dola milioni 120

**Na Renatha Msungu**

SEKTA ya Pamba nchini, iko katika hatua ya kujikwamua ishamiri katika hatua ya mafaniko. Hiyo inajumuisha ongezeko kubwa katika uzalishaji na tija kwa ekari, miongoni mwa wakulima hapa nchini.

Hatua hiyo muhimu katika uzalishaji wa zao hilo la kimkakati la kibiashara ambalo mpaka sasa limewaajiri wakulima 500,000 katika eneo la takribani ekari 1,000,000 imetokama na utekelezaji wa Mradi wa Cotton Victoria.

Mradi wa Cotton Victoria ulianza kutekelezwa katika baadhi ya mikoa inayozalisha pamba nchini, katika msimu wa uzalishaji wa mwaka 2016/2017.

Mradi huo unatekelezwa kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Brazil (ABC) kupitia Ubalozi wa Brazil nchini Tanzania, kwa bajeti ya dola za Marekani 5,802,019.08, ambao nje ya Tanzania, mradi huo pia unatekelezwa katika nchi za Kenya na Burundi.

Mpaka sasa, mradi umefanikiwa kubadilisha maisha ya wakulima wengi katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Katavi, Geita, Mwanza na mipango inaendelea kuwafikia wakulima katika mikoa mingine inayolima Pamba hapa nchini.

Wanatoa ushuhuda kwamba, baadhi ya wakulima walionufaika na mradi huo wameeleza kuwa maisha yao, yamebadilika kwa kiasi kikubwa.

"Kabla ya mradi kutufikia, nilikuwa navuna kilo 300 za Pamba kwa ekari, lakini baada ya kufikiwa na mradi na kufundishwa njia bora za upandaji na utunzaji pamba shambani kwa sasa navuna kilo 860 kwa ekari na ninatarajia kuvuna kilo 1000 msimu ujao," Samwel Marandu, mkulima wa pamba katika kijiji cha Kapanga, wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi.


Marandu ambaye kutokana na mafanikio hayo, ameweza kujenga nyumba ya kisasa ambayo hakutarajia kuimiliki katika maisha yake, akisema mafanikio hayo yamepatikana baada ya mradi kumfundisha njia ya kisasa ya upandaji pamba. Hiyo anataja ni wastani wa nafasi ya sentimita 60 kati ya mstari mmoja na mwingine na setimeta 30 shimo kati ya shimo moa na nyingine, ikiwa na idadi ya mimea inakua 44,444 kwa ekari.

Anasema awali alitumia sentimeta 22,222 kwa ekari kwa upandaji wa awali umbali kati ya shimo ni sentimita 90, aliyokuwa akiutumia.

**DC, WADAU**

Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Mkoani Katavi, Onesmo Buswelu, anafafanua kuwa tangu kuanza kwa mradi wakulima katika wilaya hiyo, wamenufaika kwa kiasi kikubwa, hali inayochangia kuongezeka a pato la wilaya kupitia biashara ya pamba. Kwa Tanzania, mradi unatekelezwa kupitia Kituo cha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Ukiliguru kilichopo Mwanza, chenue jukumu la kuratibu kitaifa shughuli za utafiti wa pamba na mazao ya mizizi kama mihogo na viazi vitamu.

Dk. Paul Saidia, ni Mkurugenzi wa Kituo hicho cha TARI Ukiliguru, anaeleza kuwa utekelezaji ... za



Samwel Marandu, mkulima wa Pamba kijiji cha Kapanga, Wilaya ya Tanganyika, Mkoani Katavi, ambaye amenufaika na mradi wa Cotton Victoria.

wa mradi umeleta mwanga mpya wa matumaini kuanzia kwa wakulima, pia zao la pamba nchini.

"Tunaishukuru serikali ya Brazil kugharamia mradi huu unaojikita katika kuendeleza zao la pamba hapa nchini," anasema Dk. Saidia, akifafanua mradi umenunua vifaa mbalimbali vya kisasa vya kulima pamba, yakiwamo matrerkta, makubwa na madogo, vifaa vya 'Power Tillers, majembe ya kisasa, vifaa vya maabara na vya kuchakata na kuongeza thamani ya pamba.

Vingine ni vifaa vya maandalizi na kupanda pamba, kutunza mbegu, kupambana na 'visumbufu', vifaa vya karakana na vitendea kazi ofisini.

**WAINGIA TABORA**

Aidha, kutokana na mafanikio ya mradi huo, serikali ya mkoa Tabora, imejiunga nao ikianza na azma ya a kutekeleza mkakati maalumu wa kuhakikisha wakulima wengi zaidi wanajikita kuzalisha pamba.

Ofisa Kilimo wa Mkoa wa Tabora, Saidi Babu, anasema pamba inalimwa na kustawi kwa wingi katika Wilaya sita Mkoani humo, ikiwemo Wilaya Igunga, Nzega, Uyui, Tabora Manispaa, Urambo na wilaya ya Kaliuwa.

"Tangu mradi wa Cotton Victoria kuanza kutekezwa hapa, tumeshuhudia wakulima wa Pamba wakipata mavuno mengi, tofauti kabisa na zamani, na hata maisha yao yamebadilika sana kiuchumi, " anashuhudia.

Anaeleza kwamba wameona ipo haja ya kuwashawishi wakulima wengi zaidi kuanza kulima pamba ili kuongeza vipato vyao na kuongeza uchumi wa mkoa kwa ujumla.

"Kwa mfano, Tabora inasifika sana kwa uzalishaji wa zao la tumbaku, lakini kwa sasa uzalishaji wa tumbaku unakabiliwa na changamoto nyingi za mabadiliko ya tabianchi, hivyo tija imeshuka na tunaona ipo haja wakulima kuanza kuwekeza nguvu zao kwenye pamba," Babu anafafanua.

Nganga Luhemeja, ni mkulima wa pamba aliyefanikiwa wa Tabora, anaeleza: "Kupitia mradi huu nimeweza kuongeza uzalishaji kutoka kilo 200 kwaekari hadi kufikia kilo 510 na ninatazamia uzalishaji kuongezeka zaidi msimu ujao."

**BALOZI & WADAU**

Balozi wa Brazil nchini, Gustavo Martins Nogueira, anasema wanafurahi kuona utekelezaji wa mradi huo wa kimkakati wanaoufadhili, umeleta mapinduzi makubwa katika zao la pamba nchini.

"Kutokana na utekelezaji mzuri wa mradi tutaendelea kuipatia Tanzania vifaa vya kisasa na fedha za kutosha, ili kuhakikisha nchi inapata matokeo mazuri zaidi katika uzalishaji wa Pamba," anasisitiza.

Dk. Furaha Mrosso ni Kaimu Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu kutoka TARI Makao Makuu ana ufafanuzi wake:

"TARI tumejipanga vyema kuhakikisha mradi unatekelezwa kwa kuakisi thamani halisi ya fedha zilizotolewa na wafadhili. Pia, wakulima lazima wanufaike kikamilifu kwa kujifunza mbinu bora ili kuendelea kuongeza uzalishaji na tija."

Wadau wengine wanaohusika katika utekelezaji wa mradi huo wa Cotton Victoria ni pamoja na Wizara ya Kilimo ya Tanzania, Taasisi ya Pamba ya Brazil (IBA), pamoja na Chuo Kikuu cha Shirikisho cha Lavras (UFLA).

Pamba ni miongoni mwa mazao ya kimkakati nchini Tanzania na zao la kibiashara, linalolimwa katika mikoa 17 na wilaya 56 nchini, ikiwajumuisha wakulima 500,000 katika eneo la takribani ekari milioni moja.

Mnyororo wa thamani wa zao la pamba unategemewa na zaidi ya asilimia 40 ya Watanzania wote na mpaka sasa, ni takribani asilimia 70 ya pamba nchini inauzwa nje ya nchi, hata kuingiza mapato ya wastani wa Dola za Marekani milioni 120 kwa mwaka.

Hali ya uzalishaji wa zao hilo nchini, inatajwa kuwa kati ya tani 122,000 hadi 370,000 kutegemea na hali ya hewa.

Uzalishaji wa pamba nchini unatajwa kuathiriwa na changamoto kama mabadiliko ya hali ya hewa, kupungua kwa rutuba ya udongo, visumbufu kama wadudu na magonjwa, kutozingatia kanuni za kilimo bora cha pamba.

Utafiti mbalimbali umefanyika na zinaendelea kufanyika, ili kuchangia kuongeza tija yake shambani, ikijumuisha ugunduzi wa mbegu bora, kanuni za kilimo bora cha pamba na kudhibiti visumbufu.

Inatajwa siri ya mafanikio hayo ya utafiti, ya zao la ushirikiano kati ya TARI, Bodi ya Pamba Tanzania (TCB) na wadau wengine.



Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Mkoani Katavi, Onesmo Buswelu, akisaidia kuvuna Pamba kwenye moja ya shamba la mkulima katika wilaya hiyo. **PICHA ZOTE: RENATHA MSUNGU.**

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tuangalie wasanii aina hii wasitupeleke gizani

UMEJITULIZA nyumbani, unaangalia televisheni baada ya kusikia kuwa mkuu wa nchi anakuwa na jambo lake punde hivi, mara unaunganishwa na kituo fulani cha luninga, unajikuta kwa macho yako unashuhudia Ikulu imesheheni.

Waliopo hapo wakijiandaa kushuhudia jambo na kumsikiliza rais na Watanzania wenzako wa kada mbalimbali, lakini wakiwamo pia wageni waalikwa wa kutoka ughaibuni na wengi ni mabalozi wakiwakilisha nchi zao.

Rais ana jambo muhimu la kushuhudia kusainiwa kwa mikataba mitatu ya uwekezaji kwenye Bandari ya Dar es Salaam kati ya Tanzania na Dubai iliyoko kwenye Umoja wa Falme ya Nchi za Kiarabu (UAE), kupitia kampuni yake ya Dubai Ports World maarufu kama DP World.





Hatua hiyo inafikiwa baada ya kupitishwa kwa Azimio la Makubaliano hayo bungeni na kufungua mjadala kwa wananchi na wadau mbalimbali, tena kwa ruhusa ya huyo huyo mkuu wa nchi na hatimaye jambo linafikia ukomo.

Maelezo ya kina yanatolewa juu ya mikataba hiyo na itatekelezwaje na ni nini kilichomo katika mikatabu husika, wahusika nao wanatia saini mbele ya macho ya mkuu wa nchi, Daktari Samia Suluhu Hassan aka Chifu Hangaya.

Ni hafla ya kufurahia, kwa maana kila aliyepo hapo anakubaliana na kilichofanyika hata kama hana maelezo ya kina, lakini ndilo linalofanyika, hivyo hapana budi kukubali na kusubiri matokeo yake katika utekelezaji.

Miongoni mwa washajihishaji wa hafla hiyo ni wasanii, yumo msanii maarufu nchini ambaye hakosi shughuli za kitaifa kama hizo, mara nyingi hupewa wasaa wa kutumbuiza na kutoa aliyonayo moyoni.

Si mwingine ni mghani, Mrisho Mpoto au Mjomba, ambaye anatambulishwa na mwendesha hafla hiyo, kutoa burudani ya wimbo maalumu kwenye mkusanyiko huo ambao nasema umekutanisha kada mbalimbali.

Kawaida yake, hughani hotuba, sijapata kumsikia akiimba bali husimulia alicho nacho, anazungumzia kinachoendelea katika Ikulu yetu mpya ya Chamwino na anajikuta mifuko inajaa noti za washiriki wa mkusanyiko huo.

Nyingi zinatoka kwa wajumbe wa kisiasa ambao punde walikuwa na kikao chao, kabla ya hicho cha mikataba.

Wakati akitambulishwa, tunaambiwa ana takwimu au data nyingi atakazotumwagia, nakuwa makini kumsikiliza ili asije akaniacha nje ya kipindi hiki kizuri cha somo la Dipiwelidi.

Wakati nanogewa na kuvutiwa na ghani zake, mara namsikia: "Mheshimiwa Rais ukitaka kujua kama jambo hili ni (si) dogo, wale wapingaji wote, kwa asilimia 95 wamekubali mwaliko wao na wako humu ndani wamekaa… umewaalika kwa sababu wameelewa, na ndiyo maana wamekubali mwaliko wako, tuko nao humu na tutakula nao mchana hapa leo."

Nashituka, utadhani alikuwa ananilenga mimi, kwa sababu ni mmoja wa wanaounga mkono uwekezaji bandarini, lakini nasigana na maudhui ya mkataba na kuomba yafanyiwe marekebisho ambayo hatimaye rais anasema yalizingatiwa.

Nikitazama mkusanyiko ule, naona baadhi ya viongozi wa dini ambao nao walifikia hatua ya kutoa tamko kupitia Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC) na tamko kusomwa kwenye makanisa yote.

Namwona Katibu Mkuu wa TEC, Padri Charles Kitima, ambaye naye bila shaka anapatwa mshituko kwa kusikia kauli ya Mpoto.



NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

Sina hakika, lakini nadhani hata mkuu naye alishituka, lakini afanyeje, kwa sababu mshale ulishaacha upinde! Basi tukaacha Mpoto aendelee kukusanya fedha za washiriki, kwani hata alipotakiwa kuacha kuendelea kughani akahimiza ziendelee ili aendelee kukusanya zao.

Kama hakuwa anafanya makusudi, basi inawezekana zile noti zilimfanya atamke vile, maneno ya kejeli na kudhalilisha baadhi ya waalikwa waliokuwa hapo kwa heshima ya Ikulu.

Pengine alichotaka kutuonesha msanii huyu, ni kwamba waliokuwa wanapinga mkataba huo hawakustahili kuwa Ikulu siku hiyo, ila waliingilia sherehe zisizowahusu, kwa ajili ya kwenda kula pale. Sijui kwa nini hakuomba radhi?

Hii ni dhana ile ile kinzani, ukipinga usipelekewe maendeleo, kama sivyo, hayo maneno aliyatoa wapi ya kunanga viongozi wakiwamo hasa wa dini, wanaostahili heshima na hata kuombea mkusanyiko ule.

Nilipoona mambo ni hayo, nikahamia kwenye mitandao ya kijamii, nikakuta kumbe waliotazama nao waliguswa na kuhoji kulikoni, wakajibiwa kwamba kumbe hata kwa baadhi ya waalikwa, mwaliko haukufafanua, wakaja kujua mengine pale pale.

Wakati nimesalia mtandaoni, ghafla nikakutana na video ya msanii mwingine wanamwita Mwemba Burton 'Mwijaku', naye ana wageni wawili mbele ya bendera za mataifa mbalimbali, anazishika na kuwapongeza wageni hao, huku akiwapapasa matumboni na kusema: "I love Pakistan, I love Tanzania, umepoa, umepoa, umepoa, nipe maokoto, nipe maokoto!"

Sikuokota kitu, nilipohoji wadau wanamjua, wakasema yuko nje ya nchi anatangaza utalii wa Tanzania kuvutia watalii. Hiyo njia anayoitumia ni yenyewe? Italeta watalii? Je ni Royal Tour Part II au kitu gani?

Niko pale nasubiri majibu yenu ndugu zangu. Wasanii hawa wa kuangalia sana!

# RC Chalamila alivyopiga saluti kwa Rais kwenye reli ya Gongolamboto

Inatoka Uk 11

usafiri ya TRC, ambayo minong'ono hasi ilishamiri, wakati huohuo Chalamila akieneza utawala bora si kwake tu, hata wakuu wa mikoa wenzake wangependa kujifunza kitu kwake.

Ndani ya siku hiyo kafanya utafiti, ikachukuliwa hatua kubwa, akiwa mwakilishi wa rais aliyependa ishara njema kwa mkuu wa nchi, aliyechukizwa na kasoro tajwa.

Baada ya kikao hicho, siku iliyofuata jana, TRC ikatangaza maboresho kutoka kasoro zilizoibuliwa na wananchi, ikiongeza safari ya ziara kuwapa ahueni wasafiri, ambayo treni ya kwenda na kurudi Pugu, itatoka saa nne usiku Gerezani, huku zkiongezwa safari tatu Jumamosi, ambazo hazikuwapo.

Nipashe katika ukaguzi wake jana ilishuhudia tija na nidhamu kubwa katika mfumo wa utendaji wa wakata tiketi katika treni, katika kashfa ya wizi wa tiketi kutumika mara mbili, aliyoambiwa Mkuu wa Mkoa.

Katika staili nyingine ya kiutendaji haki- utawala bora, Nipashe ilishuhudia namna askari polisi aliyetuhumiwa kwa uonevu juzi katika utoaji huduma stesheni, Chalamila alimhimiza Kamanda wake, Sebastian Mbuta, kuchunguza uhalali wa madai hayo, kabla ya kumchukulia hatua.

Katika jukumu lake hilo akaahidi kufuatilia kwa wiki kadhaa maboresho yaliyodaiwa kwenye treni ikiwamo kuacha namna yake ya simu kwa umma, kumfahamisha yaliyojiri na yatakayojiri, huku akiutaka uongozi wa TRC kubadilika, akisema siku hiyo katika ukaguzi alishapokea ujumbe zaidi ya 100 na alishajibu 80.

Ni somo tosha la utawala bora na biashara yenye tija kwa TRC, ambayo ni chombo ambacho ni zao la kodi ya wananchi, akionyesha tu jicho na mkono wa mkuu wa nchi, Rais Dk. Samia anapoliliwa na umma kutaka kupata 'thamani ya fedha zao katika usafiri TRC.''

UCHUMI

# Wazee – bibi wanaolea wajukuu walia umaskini, wadai mikopo ya halmashauri

**Na Sabato Kasika**



Wazee wakiwa mkutanoni. **PICHA: SABATO KASIKA**

HADI sasa katika jamii nchini, kuna Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Hiyo ni miongoni mwa chachu za kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), hasa lengo namba moja, linalogusa haja ya kutokomeza umasikini.

Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24, serikali imetenga Sh. bilioni 51, kuwezesha kaya maskini kupitia TASAF ili walengwa wapate ruzuku ya kujikimu na kuboresha maisha yao.

Hayo anatamka Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwan Kikwete, kwa walengwa wa TASAF na wananchi mkoani Singida.

Ni kipindi serikali katika mkakati kuwatetea kinamama wenye umri mkubwa maarufu 'mabibi' wanaolea wajukuu na wazazi wamekufa kwa maradhi ya Ukimwi.

Hapo nao wakatoa kilio chao, wakitamani kusaidiwa waweze kumudu maisha ya kulea na kusomesha wajukuu wao, katika jumuiko lao la siku tatu liitwalo 'International Grandmothers Gathering', lililofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Lilikuwa kundi la wazee 41 kutoka mikoa 16, chini ya mashirika ya Kimara Peer Educators &Health Promotors ya Dar es Salaam, Maasai Women Development Organization (MWEDO), wa Arusha.

Vilevile katika mikoa mingine, kunatajwa kulikuwapo vikundi vya Umoja wa Kupambana na Ukimwi (UMWI) na Rainbow Centre ya mkoani Kilimanjaro, wakiwamo pia kutoka Uganda.

Vilevile, wako kutoka nchi za Kenya, Ethiopia, Eswatin (Uswazi), Zimbabwe, Zambia, Afrika ya Kusini, Canada, Australia na New Zeland, walioshiriki kwa njia ya mtandao.

**MATESO YA UMASKINI**

Kolumba Mirau, ni kati ya kinamama wazee anasoma maelezo, akiainisha namna umasikini unavyochangia wao kufikia maisha magumu, hata wanashindwa kupata milo mitatu kwa siku.

Anaeleza kwamba, kuna wakati wanakosa baadhi ya mahitaji muhimu, wakikwazwa na kukosa kipato, hata wakishindwa kuwasomesha wajukuu zao.

"Ukija kwenye elimu, hili ni suala mtambuka, linahitaji vifaa vya shule kama madaftari, kalamu, sare na vitu vingine muhimu kwa ajili ya elimu, lakini tunakwama kutokana na ukosefu wa kipato," anasema Kolumba.

Ana ufafanuzi mwingine kwamba, kwa sasa wanakabiliwa na changamoto ya kukosa nyumba bora, hawamudu kulipa kodi ya pango na kwamba imo katika orodha ya yanayosababishwa na umaskini wa kipato.

Lingine linatajwa kuwa ni magumu kwenye taasisi za fedha kwa ajili ya kukopa fedha, hawapewi, kwa umri wao huwa wanakataliwa, kwamba hawakopesheki.

"Wakati mwingine hata hizo fedha za TASAF haziwafikii walengwa, ambao miongoni mwao ni sisi mabibi na kusababisha kuendelea kuwapo hali ngumu ya maisha kwetu tunaolea wajukuu," anasema.

Aidha, anasema ukosefu wa nishati kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, nao unasababisha wapikie samadi ambayo huwafanya wawe na macho mekundu na kunyanyapaliwa kwa kuitwa wachawi.

Kutokana na changamoto hizo, wazee hao wana maombi kwa serikali kuwasikiza na kuifanyia kazi wanayoyaomba.

**DAI ASILIMIA 10**

Kolumba anasema kutokana na uduni wa maisha yao, wanaomba waruhusiwe kupata mkopo unaotokana na asilimia 10, inayotolewa na halmashauri husika, wakiwekana vijana, bila ya kuangalia umri.

"Tunaomba tutambuliwe na serikali kama kundi maalum linalolea wajukuu walioachwa na wazazi wao, baada ya kufariki kwa janga la Ukimwi, tupate mkopo huo wa asilimia 10," anasema.

Ni maombi yanayoambatana na lingine la kutaka serikali iwezeshe upatikanaji mfumo wa pensheni maalum 'mabibi' wasioawahi kuajiriwa, lengo kuu likiwa ni kumudu gharama za maisha.

Aidha, Kolumba katika hoja ya kundi lao anawasilisha ombi serikalini la kusamehewa malipo ya tiba, kwa kuwa bado kuna kusuasua.

"Mabibi kwa miaka mingi wamekuwa nguzo kuu katika kukabiliana na athari za VVU na UKIMWI, hasa kwa upande wa kuwalea wajukuu (yatima), wamekuwa mstari wa mbele katika kukabiliana na changamoto za malezi na makuzi ya watoto," anasema.

Lingine analitaja, wamebeba dhamana kubwa, huku hawathaminiwi ipasavyo na kwamba mara nyingi hunyanyapaliwa, kutokana na sababu zilizohusishwa na vifo vya watoto wao na kwamba mazingira hayo yamewafanya wajitokeze kutoa kilio serikalini.

**UTASHI WA KISIASA**

Bibi mwingine ambaye ni Mkurugenzi wa Kimara asasi ya Peer Educators, Pfiriael Kiwia, akitoa ufafanuzi kuhusu matamko hayo, anasema utatuzi wa kero zao unahitaji utashi wa kisiasa kwa maelezo kwamba wana changamoto nyingi hazijapatiwa ufumbuzi.

"Hapa nina maana kwamba viongozi kuanzia ngazi ya chini wakiwamo wanaoshiriki katika vikao vya uamuzi, wakichukua changamoto zetu na kuziingiza katika ajenda zao tunaweza kupata unafuu wa maisha, hivyo utashi wa kisiasa ni wa muhimu katika jambo hili," anasema Pfiriael.

"Wanapotajwa wazee, watu hudhani kuwa ni kiume tu, huku wa kike wanaolea wajukuu wakiachwa pembeni, lakini ninaamini kwamba utashi wa kisiasa unaweza kusaidia kumaliza yanayotukabili," anasema.

Anasema mabibi wanaolea wajukuu katika nchi, wapo wengi na kwamba wanaendelea kukusanya takwimu zao, ili kupata idadi kamili na kwamba wakiwa katika harakati hizo wanatoa yao yawafikie watunga sera, kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalum ili waone umuhimu wa kuboresha maisha ya mabibi hao.

Doreen Mawala kutoka shirika la UMWI, anasema wameamua kupaza sauti ili serikali isikie kilio chao na kukitafutia ufumbuzi.

"Wabibi wamebeba majukumu mazito ya kulea wajukuu, huku wakiwa hawana kitu cha kuwawezesha kuhudumia watoto hao na wao wenyewe," anasema Doreen.

Anasema bila kupaza sauti, wataendelea kuumia, kwa kuwa wao ni kundi ambalo ni kama limesahaulika ingawa limebeba jukumu la kulea wajukuu bila msaada.



## HABARI DODOMA

# Kiwango tatizo la kisukari chaongezeka nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema kwa sasa kuna kiwango kikubwa cha Watanzania wenye tatizo la ugonjwa wa kisukari na inakisiwa watu 12 kati ya 100 wana ugonjwa huo.

Aidha, amesema wiki mbili zijazo wizara inatarajiwa kuzindua mwongozo wa ulaji chakula unaofaa ili kuondokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Ummy alitoa kauli hiyo jana jijini hapa katika hafla ya makabidhiano ya magari tembezi (kliniki tembezi) yaliyotolewa na Taasisi ya Huduma za Afya ya Agha khan Tanzania na Serikali ya Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW), yenye thamani ya Sh. milioni 620.

Alisema takwimu za mwaka 2012 zilikuwa zinaonesha asilimia tisa katika kila watu 100 wa miaka 15 na kuendelea, watu tisa wana ugonjwa huo.

"Mwezi Desemba, mwaka huu, tutapata takwimu mpya inakisiwa ni watu 12 katika kila watu 100, mtaona ongezeko la wagonjwa wa kisukari, lakini pia tuna changamoto ya wagonjwa wa shinikizo la juu la damu takwimu zinaonesha asilimia 25 na watu hawajui," alisema.

Alitaka magari hayo yatumike kukabiliana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

"Tuna changamoto ya kifua kikuu kuwaibua karibu asilimia 35 ya wagonjwa wa kifua kikuu bado tunao kwenye majumba yetu, ofisi zetu kwa hiyo naamini magari haya yatatumika kwenye mapambano ya kifua kikuu," alisema.

Alisema pamoja na kutoa huduma ya kuhamasisha chanjo ya Uviko-19 pia magari hayo yatatumika huduma za chanjo kwa watoto.

"Nasisitiza magari haya yakatumike kwenye mapambano ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza, muende kwenye maeneo ya mkusanyiko wa watu kwa mfano sokoni muwapime sukari," alisema.

Kuhusu matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango, alisema pia kliniki hizo zihamasishe masuala ya uzazi wa mpango.

"Sisi kama sekta ya afya hatupaswi kuwaambia watu wasizae, ni vizuri watu wakapanga uzazi kwasasa watu wa mjini wapo kwenye watoto wa tatu, lakini Kanda ya Ziwa huko Simiyu unaona kiwango kimeenda sita hadi nane," alisema.

Naye, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kanda wa Taasisi ya Huduma za Afya za Aghakhan, Afrika Mashariki, Dk. Zeenat Suleiman, alisema moja ya malengo ya taasisi hiyo ni kuendelea kuboresha utoaji huduma na magari hayo yamenunuliwa kupitia mradi wa chanjo ya Uviko-19.

Aliahidi taasisi hiyo itaendelea kushirikiana na serikali kuboresha huduma za afya na kuwafikia wananchi waishio vijijini.




Diwani wa kata ya Matumbulu, jijini Dodoma, Emmanuel Chibago akichangia hoja akiitaka Halmashauri ya Jiji hilo, kutekeleza miradi iliyoahidiwa kwenye kata hiyo, kwenye kikao cha kawaida cha robo mwaka cha Baraza la Madiwani jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mameneja RUWASA watakiwa kutoa elimu miradi maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amewaagiza mameneja wa mikoa na wilaya wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kuwashirikisha maofisa Maendeleo ya Jamii katika hatua zote za utekelezaji wa miradi ya maji ili kutoa elimu kwa jamii.

Alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya siku mbili ya kuwajengea uwezo maofisa hao kuhusu utoaji huduma endelevu ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

"Watendaji wote kuanzia ngazi ya wizara, mikoa na wilaya washirikisheni Maofisa Maendeleo ya Jamii katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini ili wawe sehemu ya malengo ya wizara katika kufikia asilimia 85 ya upatikanaji wa majisafi vijijini ifikapo mwaka 2025 na waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi," alisema.

"Mimi Waziri wa Maji nipo pamoja nanyi Maofisa Maendeleo ya Jamii kwa kuwa maendeleo ya sekta ya maji yanaanza na wewe na sisi sote, unyonge basi tukafanye kazi."

Alisema hakuna taasisi iliyofanikiwa kwa uongo na kutaka kuwapo na ushirikiano ili miradi ijengwe kulingana na thamani ya fedha iliyotolewa.

"Hakuna taasisi yoyote iliyofanikiwa kwa uongo, wakati mwingine taasisi inakufa inashindwa kufikia mafanikio watu wanaumizana sana, twendeni tukafanye kazi kila mmoja atimize majukumu yake, kasimamieni miradi," alisema.

Aidha, aliipongeza RUWASA kwa usimamizi mzuri wa Miradi ya Maji ya Matokeo kwa Malipo (P4R), Tanzania ikiwa kinara duniani kwa usimamizi na utekelezaji huo.

# EWURA yapewa meno kusimamia mafuta bila woga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ameitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kusimamia sekta ya mafuta kwa ufanisi na kutoogopa kutuhumiwa au kutishwa na watu.

Aidha, aliahidi serikali itaharakisha kukamilisha kanuni za sekta ya mafuta.

Akizindua jana Baraza la Pili la Wafanyakazi wa Mamlaka hiyo jijini hapa, Dk. Biteko aliipongeza EWURA kwa kushusha bei za mafuta na kuwataka wasiogope kutuhumiwa au kutishwa na watu badala yake wasimamie sekta hiyo kwa ufanisi.

"Nawaahidi kanuni za eneo la mafuta tutaharakisha ili zikamilike, nitahakikisha hamkwami, lakini msivute miguu maana kuna hatari kubwa bali simamieni hii sekta ili iwe tulivu na taasisi imara zaidi," alisisitiza Dk. Biteko.

Alielekeza EWURA kupitia upya gharama za uagizaji wa mafuta ambazo awali zilikuwa kubwa na kusababisha athari mbalimbali ikiwamo kuongezeka kwa gharama katika sekta ya usafirishaji na uzalishaji.

"Gharama hizi za uagizaji mafuta zilikuwa kubwa mno huku kukiwa hakuna sababu ya kuwa kubwa kwa kiasi hicho, niliwapa maelekezo mkazitazame upya, nashukuru mmeziangalia na nina furahi kwamba zimeshuka na hivyo kupunguza makali kwa watumiaji," alisema.

Aidha, aliwataka watendaji na watumishi wa EWURA kuzingatia maslahi ya Watanzania na maslahi ya nchi katika kazi zao za udhibiti wa huduma za nishati na maji ili Watanzania wapate huduma bora na kwa gharama nafuu.

"Watumishi wekeni mkazo katika kudhibiti vitendo vya urasimu na rushwa mahali pa kazi, kuangalia maslahi binafsi wakati wa kutenda kazi, huku tukiwauliza Watanzania walio wengi ambao sisi ni sehemu yao."

"Tukimuona mtu yeyote anatumia cheo chake hapa EWURA kuwatisha watu, kukusanya rushwa, huyo tumuone ni adui yetu wote, na tumkemee, tusisubiri Mkurugenzi achukue hatua au bodi," alisema.

Aliwahimiza kufanya kazi kwa weledi, ubunifu unaoendana na kasi ya teknolojia na maendeleo ya dunia kwa kuwa taifa lina mategemeo makubwa na watendaji hao. Aliwasisitiza wafanyakazi hao kuwajibika ipasavyo katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuhakikisha watoa huduma wanafanya ushindani wenye tija na ufanisi kiuchumi, kulinda maslahi ya walaji na mitaji ya kifedha ya watoa huduma pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa huduma kwa makundi yote ikiwamo vijijini.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile, alisema kuwa taasisi hiyo imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ili huduma za nishati na maji zipatikane kwa uhakika, kutosha, uendelevu na gharama ambazo wananchi wanazidumu.

Alisema, ajenda za baraza hilo zitatoa tathmini halisi ya utendaji wa Mamlaka kwa mwaka uliopita na kutoa fursa ya mawazo na namna bora ya kuboresha utendaji kama taasisi kwa miaka ijayo katika kutimiza malengo ya kitaifa.





Mmoja wa wakazi wa kijiji cha Matwiga, wilayani Chunya mkoani Mbeya, akichota maji kwenye moja ya vituo vya mradi wa bwawa la Matwiga jana, ambao umeanza kutoa huduma baada ya miaka 17. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Chuo NACTIVET chasimamishwa kwa kukiuka masharti ya usajili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTIVET), imekisimamisha Chuo cha Mbeya Training College cha jijini Mbeya kutokana na kukiuka masharti ya usajili ikiwamo kutoa mafunzo ya fani ambazo hakijaruhusiwa.

Aidha, baraza hilo limetoa siku saba kwa uongozi wa chuo hicho kujieleza kabla hakijachukuliwa hatua kali zaidi ikiwamo kufutiwa usajili kutokana na ukiukwaji wa taratibu hizo.

Chuo hicho kilisimamishwa juzi wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mbeya na maofisa wa NACTIVET Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilipofanya kikao na uongozi wa chuo hicho pamoja na wanafunzi.

Meneja wa NACTIVET Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Joha Zabron, alisema chuo hicho kilisajiliwa mwezi Februari, mwaka huu kwa ajili ya kutoa fani za wahudumu wa hoteli, makatibu muhtasi, wataalamu wa kompyuta na maofisa biashara.

Hata hivyo, alisema kimekiuka masharti ya usajili wake kwa kuanza kutoa kozi za afya ikiwamo ya wataalam wa maabara huku baadhi ya wanafunzi waliosajiliwa wakiwa hawajaomba na hawana sifa za kusoma kozi hiyo.

"Katibu Mtendaji wa NACTIVET, ameelekeza tuchukue hatua kwa kusitisha mafunzo kwenye chuo hiki kwanza kwa hatua za awali, hatua inayofuata ni wamiliki kujieleza kwa nini tusikifutie kabisa usajili chuo hiki," alisema Zabron.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alisema kwa mujibu wa taarifa alizozipata baadhi ya wanafunzi waliosoma kozi hizo katika chuo hicho hawana sifa za kuajiriwa kutokana na vyeti vyao kutambuliwa na taasisi za ajira.

Alisema vyeti hivyo vilivyotolewa na chuo hicho vinatambuliwa kama feki na wamiliki wa chuo hicho wamekiuka miiko na taratibu za usajili hali ambayo inaleta uhalali wa kufungiwa. Aliwataka maofisa wa NACTIVET na VETA kufanya ukaguzi wa vyuo vyote vilivyomo ndani ya wilaya hiyo na kuchukua hatua kwa vyote vitakavyobainika kukiuka taratibu za usajili.

"Hakuna mzazi hata mmoja ambaye angependa safari ya maisha ya mtoto wake yawe kama haya ambayo yanafanywa na chuo hiki, sasa sisi tupo hapa kwa ajili ya kuhakikisha tunachukua hatua na kila mmoja anapata haki yake," alisema Malisa.

Alisisitiza kuwa wamiliki wa chuo hicho watachukuliwa hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine ambao wanafanya makosa kama hayo.

Aliagiza Jeshi la Polisi kumkamata mmiliki wa chuo hicho na kumweka ndani ili hatua zingine za kisheria zianze kuchukuliwa dhidi yake na wazazi wapate haki.

Baadhi ya wazazi walilalamika kuwa wamewalipia ada watoto wao kwa muda wa miaka miwili na wakahitimu, lakini hawakubaliki kwenye ajira kutokana na vyeti vyao kutotambuliwa.

# Vijiji sita vyanufaika maji ya Bwawa la Matwiga

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MRADI wa Bwawa la Maji la Matwiga, wilayani Chunya, uliokuwa umekwama kwa zaidi ya miaka 17 umeanza kutoa huduma kwa wananchi wa vijiji sita kati ya 16 vinavyotarajiwa kunufaika na mradi huo.

Mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2006 na ulilenga kuhudumia vijiji 16 vya kata za Matwiga, Lualaje, Lupatingatinga, Mtanila na Kambikatoto, lakini umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu kutokana na sababu mbalimbali.

Juzi, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya, ilifanya ziara katika mradi huo kwa lengo la kukagua utekelezaji wake na kukuta umekamilika na baadhi ya maeneo wananchi wameanza kupata huduma huku maeneo mengine wakiendelea na ujenzi.

Meneja wa Wakala wa Usambazaji wa Maji Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Chunya, Mhandisi Oleneno Sanga, alisema kwa sasa mradi huo umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na wananchi wameshaanza kupata huduma.

Alisema katika awamu ya kwanza mradi huo umeanza kuhudumia vijiji sita ambavyo vimejengewa miundombinu yote muhimu na kuundiwa chombo maalumu cha uendeshaji.

"Tumejenga vituo 36 vya kuchota maji kwenye jumuiya na vyote vinatoa huduma, baadhi ya vijiji ambavyo vinapata huduma ni pamoja na Matwiga, Mazimbo na Isangawana na idadi ya wananchi wanaopata huduma ni 20,000," alisema Mhandisi Sanga.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Hance Patrick, alisema wanasubiri kupata fedha zingine kutoka wizarani kwa ajili ya kukamilisha maeneo yaliyobaki kwenye mradi huo ili wananchi wa vijiji vilivyobaki vianze kunufaika.

Alisema baadhi ya maeneo yamekamilika kwa asilimia 100 na mengine yamefikia zaidi ya asilimia 90 na fedha zikishapatikana watakamilisha haraka kwa kuwa sasa mradi huo unatekelezwa na mafundi wa RUWASA kwa kutumia akaunti ya dharura.

Alisema tatizo kubwa linalowakabili ni ucheleweshaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo na ndiyo sababu iliyofanya uchelewe.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alisema licha ya mradi huo kuwa na faida kubwa kwa wananchi, umekuwa ukikabiliwa na tatizo la uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za kibinadamu.

Alisema baadhi ya shughuli ambazo zimekuwa zikichangia uharibifu wa mazingira hayo ni ufugaji pamoja na ukataji miti ovyo kwa ajili ya kuni, kilimo na ujenzi wa makazi mapya.

"Kwa sasa uharibifu huu wa mazingira angalau umeanza kupungua kwa sababu tulishatoa maelekezo kwa viongozi wa vijiji kuwachukulia hatua waharibifu hao wa mazingira," alisema Mayeka.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliagiza mifugo yote iliyopo maeneo hayo ya chanzo cha maji na mengine ya hifadhi iondolewe ili mradi huo uwe endelevu.

Alisema atawasiliana na Waziri wa Maji kumuomba ili fedha za kukamilisha mradi huo zitolewe haraka na ujenzi ukamilike na wananchi waanze kunufaika.

# Wasimamizi miradi waagizwa kulipa mafundi kwa wakati

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WASIMAMIZI wa miradi ya serikali mkoani Njombe, wametakiwa kuwalipa mafundi wanaotekeleza miradi hiyo kwa wakati ili kuepuka kusababisha wizi wa vifaa kwenye miradi husika.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Njombe, Kassim Ephrem, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa.

Alisema mafundi wanapofanya kazi za serikali na kuacha shughuli zingine na kushindwa kulipwa kwa wakati kunaweza kuchangia wizi wa vifaa vya miradi katika siku zijazo.

"Mfano mafundi wanalalamika hatujalipwa malipo yetu, tunaamini kabisa kitendo cha fundi kuacha kazi zake na kuja kufanya kazi za serikali halafu hamjamlipa inamkatisha tamaa na hayo yanaashiria huko tuendapo hata wizi wa vifaa kwenye mradi," alisema Ephrem.

Alisema kama serikali imetuma fedha kwenye mradi hakuna sababu ya kushindwa kuwalipa mafundi hao ili wafanye kazi hiyo kwa viwango na uaminifu mkubwa.

Pia, katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Julai mpaka Septemba, mwaka huu, taasisi hiyo imefuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo 39 yenye thamani ya Sh. 36.3.

Alisema kati ya miradi hiyo 31 ni kutoka sekta ya elimu, mitano kwenye sekta ya afya na mitatu, sekta ya maji ambayo kwa pamoja inagharimu kiasi hicho cha fedha.

Hata hivyo, alisema miradi 12 kati ya hiyo yenye thamani ya Sh. bilioni 12. 1 ilibainika kuwa na upungufu na hatua mbalimbali zimechukuliwa kurekebisha.

Pia, aliwataka mafundi mkoani hapa kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ili iweze kukamilika kwa wakati kabla ya mvua kuchangamka.

Mkuu wa TAKUKURU wilaya ya Wanging'ombe, Scholastica Assey, alisema ili kuendelea kupambana na rushwa, wananchi wanatakiwa kutoa ushirikiano wanapotakiwa kutoa ushahidi mahakamani.

"Kwa zile taarifa ambazo mtu unatakiwa kusimama mahakamani wawe tayari kwa kuwa kesi hiyo ni ya Jamhuri usipotoa ushahidi kesi hiyo haina maana," alisema Assey.

Mmoja wa wananchi mjini Njombe, Enoky Mhagama, alisema TAKUKURU iendelee kutoa elimu kwa wananchi ili wajue namna ya utoaji wa taarifa juu ya uwapo wa matukio ya rushwa na kutoa ushirikiano anapohitajika mahakamani.

# Bei za petroli, dizeli zapaa mafuta ya ndege nayo juu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BEI ya petroli, dizeli, mafuta ya taa na ya ndege visiwani hapa yameongezeka bei mwezi Novemba, sababu ni kuongezeka kwa gharama za nishati hiyo katika soko la dunia.

Akitangaza bei za mafuta, kwa waandishi wa habari jana, Meneja wa kitengo cha uhusiano kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mbarouk Hassan, alisema pia sababu zingine ni kuongezeka kwa gharama za uingizaji wa mafuta na kuongezeka kwa wastani wa thamani ya dola.

Alisema mafuta ya petroli kwa mwezi huu yameongeza kwa Sh. 186 sawa na asilimia sita ambazo kuanzia jana yameuzwa lita moja kwa Sh. 3,187 na bei ya mwezi wa Oktoba ilikuwa Sh. 3,001.

Alisema dizeli inauzwa lita moja kwa Sh. 3,323 ongezeko la Sh. 41 sawa na asilimia moja ikilinganishwa na bei ya Oktoba ambayo ilikuwa Sh. 3,282.

Aidha, alisema mafuta ya taa lita moja ni Sh. 3,300 ongezeko la Sh. 378 sawa na asilimia 13 ikilinganishwa na bei ya Oktoba ambayo ilikuwa 2,921 na mafuta ya ndege yanauzwa lita moja Sh. 2,976 ongezeko la Sh. 208 sawa na asilimia nane ikilinganishwa na mwezi wa Oktoba ambayo ilikuwa Sh. 2,768.

Aliwataka wananchi kununua mafuta katika vituo halali na kudai risiti za kiektroniki kwa sababu risiti ndio itakayomsadia kupata fidia au haki yake ikiwa atapata changamoto yoyote.

Hata hivyo, alisema mvua kubwa iliyonyesha siku tatu mfufulizo wiki iliyopita imesababisha athari kwa baadhi ya vituo vya kuuzia mafuta baada ya maji ya mvua kufurika kwenye baadhi ya vituo.

"Mamlaka tumefanya ukaguzi wa vituo vyote ambavyo vilipata hitilafu na kupima mafuta na tulipokea malalamiko kutoka kwa wanachi kuwa mafuta yamechanganyikana na maji," alisema.

Alisema kwa bahati mbaya wananchi waliolalamika hawakuwa na risiti ya ununuzi wa mafuta licha ya mamlaka kugundua kuwa kuna kituo kimoja mafuta yalichanganyika na maji, lakini mwananchi alishindwa kulipwa fidia kwa sababu ya kutokuwa na risiti.

Alisema mamlaka ilichukua hatua ya kulifungia tangi la mafuta lililochanganya na maji katika kituo hicho ambacho hakutaka kukitaja, hadi mafuta yalipotolewa na kufanya marekebisho ya kuweka mafuta safi na kuyauza.

Baadhi ya wananchi wakizungumza na Nipashe kuhusu kupanda kwa bei hiyo, walisema kuwa muhimu mafuta yawepo ili shughuli za kiuchumi na kijamii zisisite, lakini pia serikali iangalie njia mbadala ya kupunguza bei ya nishati hiyo.

"Kwa kweli bei ya mafuta ni kubwa, lakini tunashukuru kwamba yapo hakuna uhaba wa mafuta maana kungekuwa na uhaba ndio ingekuwa balaa kubwa maana baadhi ya huduma muhimu zingesita," alisema Rashid Ali mkazi wa visiwani hapa.

Muhammed Khatib dereva wa Bodaboda, alisema ongezeko la bei hiyo litaleta athari kubwa ya kiuchumi kwa sababu kupanda kwa bei ya nishati hiyo itasababisha kupanda kwa mfumko wa bei kwa baadhi ya bidhaa.




Mkurugenzi Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Dk. Salum Khamis (kulia), akikabidhi visaidizi vya watu wenye ulemavu kwa Mwakilishi wa Zanzibar Maisha Bora Foundation, Mohamed Nyahega katika ukumbi wa Nyumba za Wazee Sebleni, Unguja jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SUZA yaagizwa kukamilisha mradi maendeleo ya elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Mwanaasha Khamis Juma, amewataka watendaji wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kukamilisha kwa wakati mradi wa maendeleo ya elimu ya juu kwa mabadiliko ya kiuchumi Zanzibar (HEET) ili kuleta tija kwa vijana wa elimu ya juu.

Alisema hayo jana chuoni hapo, Tunguu nje ya mji wa Zanzibar wakati wa majadiliano ya maendeleo ya mradi huo kwa wajumbe wa bajeti wa Baraza la Wawakilishi.

Alisema malengo ya kamati ya bajeti kufika hapo na kujadili juu ya mwelekeo ya mradi huo ni kutaka kufahamu kama kuna changamoto zozote ili zitatuliwe na mradi huo umalizwe kwa wakati na kwa ubora ili wanafunzi wanufaike.

Alisema Serikali ya Zanzibar inapoomba fedha kwa wahisani kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wake ni vyema mradi huo ukamilike kwa wakati na fedha zitumike ilivyokusudiwa ili wafadhili wa miradi waridhike na kinacho fanywa.

Alisema kuwa katika kufikia maendeleo na malengo ya mradi huo lazima wasimamizi wa mradi huo wajitume zaidi na kushirikiana na vyuo vingine ili kufikia malengo ya serikali na kuwa na tija kwa walengwa.

Alisema ikiwa mradi huo unatekelezwa Tanzania na Zanzibar kwa baadhi ya vyuo vya elimu ya juu, lazima kuwe na ushindani wa ubora wa kukamilisha majengo ya mradi na mazingira kuwa mazuri.

Wakichangia ripoti ya mradi huo wajumbe wa kamati hiyo walisema licha ya kuonekana kuwa mradi huo unaenda kukamilika mwaka 2026 bado majengo hayaja jengwa kwa wakati ni lazima kukaa na washauri elekezi na kuanza ujenzi huo.

Rukia Ramadhan Mapuri ni miongoni wa wachangiaji hao, ambaye alisema kukamilika kwa mradi huo kutatoa fursa kwa vijana wanoingia katika masomo ya elimu ya juu kuwajenga kuwa watafiti wazuri wa fani mbalimbali.

Alisema mradi umeonesha nia ya kujengwa kwa dahalia ya wanafunzi elfu moja katika kampasi ya SUZA na kuondoa changamoto za wanafunzi na kuwapa utulivu wa kusoma na kufanya mitihani yao vizuri.

Naye Makamu Mwenyekiti wa SUZA, Profesa Mhammed Makame Haji, alisema mradi huo unatekelezwa Tanzania nzima ambao Zanzibar chuo hicho pekee kimebahatika, na malengo ya mradi ni kukarabati majengo na kutengeneza majengo mengine matatu ikiwamo jengo la chuo cha kilimo pamoja na dahalia kwa wanafunzi wa kike na wa kiume pamoja na ujenzi wa maabara.

Alisema mradi huo utakapokamilika utazalisha vijana bora katika fani mbalimbali hasa katika kilimo na utafiti wake na ndiyo lengo la serikali kuwa na wasomi wazuri na watafiti.

Akiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa mradi huo, Naibu Mwenyekiti wa chuo hicho, Dk. Hamza Chanda, alisema mradi huo umeainisha ujenzi wa miundombinu mitatu kwa majengo ya ghorofa matatu ambayo ni maabara ya kisasa ya sayansi dahalia ya wanafunzi ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1000 na jengo la chuo la kilimo. Majengo yote yatagharimu Sh. bilioni 33.4.

# EMAT wakumbushwa kutoa huduma kwa ufanisi, weledi

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wafanyakazi wa huduma za tiba za dharura Tanzania (EMAT), watendaji na wadau wa Sekta ya Afya nchini wametakiwa kuchukua jitihada zaidi kwa kufanya kazi kwa ufanisi na weledi ili ufahamu na uelewa wa taaluma ya huduma za afya za dharura kuwafikia wananchi wengi.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, aliyasema hayo wakati akisoma hotuba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussen Ali Mwinyi, katika ufunguzi wa mkutano wa tano wa huduma za tiba za dharura uliofanyika juzi, visiwani humo.

Alisema wataalamu wa huduma ya tiba ya dharura wanapaswa kuwa tayari kutoa tiba sahihi inapohitajika ili kupata matokeo chanya ya kuokoa maisha yanapotokea majanga ya dharura.

Alisema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama nchi nyingine duniani hakuna kinga ya kutokupata dharura kama vile majanga ya ajali na vifo vinavyotokana na ajali za barabarani na majanga mbalimbali yanaendelea kupoteza maisha au kuwaachia ulemavu wa kudumu wanachi na kwamba ni lazima kujiandaa kukabiliana na majanaga ya aina yoyote ambayo yanaweza kutokea.

Hemed aliwataka washiriki wa kongamano hilo na wadau wa sekta ya afya kuwa tayari kuleta ufanisi wa matibabu ya huduma za dharura, serikali zote mbili zimeanzisha mfumo wa kutoa huduma za hizo.

Aidha, SMZ na SMT kwa kuona umuhimu wa kuwa na mfumo imara wa kutoa huduma za tiba za dharura katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini pia imejenga na kuweka vifaa kwenye idara 119 za tiba za dharura Zanzibar, hospitali 10 za wilaya, na hospitali moja ya mkoa tayari zinatumia mfumo huo.

Alisema serikali imeamua kuweka idara ya tiba ya dharura 14 kutoka idara mbili kwaka 2021/2021 lengo ni kuipa kipaumbele idara hiyo ni kupunguza vifo na ulemavu wa kudumu kwa wananchi inapotokea dharura kama vile ajali na nyinginezo.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, aliwataka wanafunzi wanaomaliza masomo yao ya sekondari kusomea kada ya huduma ya tiba za dharura ambayo ina uhaba mkubwa wa madaktari wabobezi wenye uwezo wa kutoa huduma za haraka hasa katika kuokoa maisha ya wananchi ambao hupatwa na majanga yasiyotarajiwa.

Alisema kuwa Wizara ya Afya Zanzibar kwa kushirikiana na EMAT imeawaalika wadau tofauti kwa lengo la kubadilisha na uzoefu na taaluma ili kuleta ukuaji wa haraka wa huduma za dharura na kupata ujuzi na suluhisho za changamoto la ongezeko la vifo vinavyotokana na majanga.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

FORM 58
IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE
AT ONE STOP CENTRE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1121 OF 2023
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE
MWAJUMA BANANA MASANJA
AND
IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY LIMBE SYLVESTER MASANJA

GENERAL CITATION
(Rule 75)

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **23 day of 11, 2023.**
Dated at **DAR ES SALAAM** this 16 Day of 10, 2023

---

REGISTRATION OF DOCUMENTS ORDINANCE
(CAP. 117)
CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL

**THIS CHANGE OF NAME DEED** is made this **2nd day of June 2022** by me **JANETH SHIJA NSENGWA** or sometimes as **JANETH PAULINE SHIJA**, formerly names known as **JEANETHE SHIJA NSENGWA**, or sometimes as **PAULINE JEANETHE SHIJA** of Post Office Box Number 75254 a resident of Dar es salaam, now or until recently called **JANETH SHIJA NSENGWA** or sometimes as **JANETH PAULINE SHIJA.**
**WITINESSES AND IT IS HEREBY DECLARED** as follows:

- I absolutely renounce and abandon the use of my said former names of **JEANETHE SHIJA NSENGWA** and **PAULINE JEANETHE SHIJA,** and I assume and determine to take and use the new name **JANETH SHIJA NSENGWA** and **JANET PAULINE SHIJA** of in substitution of my former names **JEANETHE SHIJA NSENGWA,** of and as **PAULINE JEANETHE SHIJA.**
- **AND IN PURSUANCE** of such change of name (s) as aforesaid **I DECLARE I** shall at all times hereafter in all records, documents and other writings and in all actions and dealings and on all occasions whatsoever use the new name of **JANETH SHIJA NSENGWA and JANET PAULINE SHIJA** in substitution for my former names of **JEANETHE SHIJA NSENGWA** and **PAULINE JEANETHE SHIJA** so relinquished as aforesaid to the intent that I may hereafter be known not by the aforesaid former names, but by the new names **JANETH SHIJA NSENGWA and JANET PAULINE SHIJA** as known as one person.
- **ANDI I HEREBY AUTHORISE AND REQUIRE** all persons at all times to describe and address me by the new names of **JANETH SHIJA NSENGWA** and **JANET PAULINE SHIJA.**

**IN WITNESS** whereof I have hereunto subscribed my new names of **JANETH SHIJA NSENGWA** and **JANET PAULINE SHIJA,** and have affixed my signature the day and year herein written.



---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAMES JOHN ZAIT** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye jina PASSIONIST FATHERS namba za usajili T676ACP aina ya Landrover 110, Chassis No. SALLDHHF7-LA935005, Engine No. 11L38466A. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DOD/DOD/8205/2023.**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA LILILOPO BUKOBA KAGERA
MAOMBI MADOGO NA. 55/2023 (Yatokanayo na Maombi Na. 07/2023 katika Baraza la Wilaya Bukoba)
DR. PROJESTUS KWEYAMBA.........MWOMBAJI
DHIDI YA

- **GLORIA FRANCIS**
- **MEDARD DAUDI MWIJAGE.........WAJIBU MAOMBI**

**KWA: GLORIA FRANCIS NA MEDARD DAUDI MWIJAGE**

**(POPOTE PALE MLIPO)**
Mnaarifiwa kuwa Maombi madogo Na. 55/2023 yamepangwa kutajwa tarehe 15/11/2023 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza P. J. Makwandi saa 2:00 asubuhi. Hivyo, mnaamuriwa kuhudhuria nyinyi wenyewe/mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hii leo tarehe 11/10/2023.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - BUKOBA**

---

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
IN THE DISTRICT REGISTRY
AT MUSOMA
MISC. LAND APPLICATION NO 64 OF 2022
(Arising from land Application no 21 0f 2020 at the Dlht Musoma at Musoma
CHACHA NYAGEKO......................APPLICANT
VERSUS
1. BHOKE NENGA GAIBE
2. BOROYE NKORORO
3. WEREMA MWITA SINGURI...............RESPONDENTS

**TO: Bhoke Nenga Gaibe**
**c/O v.e.o Rung'abure village**
**P.O.Box 126**
**Serengeti.**

**SUMMONS FOR PUBLICATION**
**WHEREAS** the application have filed an application against you, you hereby summoned to appear in this court in person or by pleader duly instructed and able to answer all material queation relating to the appeal or who shall be accompanied by some person able to answer all such questions on the 20th day of MARCH 2024 at 9:00 am o'clock in the forenoon before Hon, F.H.MTULYA,Judge to answer the case.
Take notice that in default of your appearance on the day before mentioned,the suit will be heard and determined in your absence.
Given under my Hand and seal of the court this 2nd day of november 2023

**Ag.DEPUTY REGISTRAR**
**MUSOMA**

---

## KUPOTEA KWA NYARAKA ZA UMILIKI WA KIWANJA

**HAMIS ALLY BWATANI** anatangaza kupotelewa na Nyaraka ya Umiliki wa Kiwanja namba 300 Kitalu 'HH' kilichopo Ndala Manispaa ya Shinyanga.
Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Hamis kwa simu namba 0754048250.
Taarifa ya Polisi RB:
PHQ/SHI/SHI/1048/2023.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHOMALI SAIDI ALLY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye jina PETER GWIDO KASUGA namba za usajili T578AVU aina ya Toyota Landcruiser. Chassis No. KJZ780030240, Engine No.1KZ0190869.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi:
**PHQ/DOD/DOD/8127/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MENRAD HUBERT RWABUTAZA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA PREMIO yenye jina la umiliki MENRAD HUBERT RWABUTAZA, namba ya usajili T 108 BKT, CHASSIS NAMBA: ZZT2400008740 na ENGINE NAMBA: 1ZZ0949865. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/31151/2023.**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA
WILAYA YA MOROGORO
MKOA WA MOROGORO
Usimamizi wa Mirathi Na......59/2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU: KASSIMU KEBERO WA KIEGEA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA NA ASHURA BALAGULA
TANGAZO
(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 13 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia.

Imetolewa leo tarehe 06 mwezi 11 mwaka 2023

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DALGHA MAKSUD SHINGANYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 806 BRZ aina ya Suzuki Escudo, Chassis namba TD52W103004 na Engine namba J20A118444.
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
TAARIFA YA POLISI
**PHQ/MAN/ BAB/1848/2023**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOYCE EDWARD MMBAGA**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 832 BXT. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/ARU/ARU/6681/2023.**

---

## TANGAZO LA MNADA

Held auctioneer Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Gari Mjini Dodoma Mteja anashauriwa kulipa deni ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Bonipeter Edward Mlaki | LandRover Rangerover T279DNU | 25.11.2023 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa Mawasiliano Piga 0677014355(Fanikiwa) 0713197485(Held auctioneer)**

---

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Baba wa kipalestina akiwasaidia watoto wake kukimbia mashambulizi yanayofanywa na ndege za Israel jana. **PICHA: AFP**

# Israel yadai Wapalesina 50,000 waondoka Gaza Kaskazini

**TEL AVIV, Israel**

JESHI la Israel limesema Wapalestina 50,000 wamekimbia kaskazini mwa Gaza na kuelekea kusini mwa eneo hilo kuanzia juzi.

Taarifa hiyo ilitolewa jana wakati mapigano makali yakiendelea ndani ya Gaza.

Msemaji wa jeshi, Daniel Hagari alinukuliwa akisema wameshuhudia wakazi hao wa Gaza wakiondoka kwa sababu wanajua tayari Hamas imepoteza udhibiti katika eneo la kaskazini na kwamba eneo la kusini liko salama zaidi.

Aliongeza kuwa hawatasitisha mapigano dhidi ya wanamgambo wa Hamas, lakini wataruhusu usitishwaji wa mapigano katika nyakati fulani ili kutoa nafasi kwa misaada ya kiutu kuwafikia raia waliokimbilia kusini mwa Gaza.

Jeshi hilo awali lilisema liliharibu mahandaki 130 ya wanamgambo wa Hamas tangu mzozo huo ulipoibuka mwezi mmoja uliopita.

Kulingana na jeshi hilo, wanamgambo wa Hamas wana mtandao mkubwa wa mahandaki ya chini ya ardhi katika eneo la Ukanda wa Gaza.

IDF ilichapisha video zilizoonyesha vifaa vikichimba maeneo ya kuingia kwenye mahandaki na kuondoa vifuniko vilivyotengenezwa kwa saruji na kukuta vifaa vya kusambazia maji, hali iliyodhihirisha kwamba wanamgambo hao walikuwa wamejiandaa kukaa kwenye mahandaki hayo kwa muda mrefu. Baadhi ya mahandaki pia yalikuwa na umeme.

Mahandaki hayo yalikuwa na urefu wa mita mbili na upana wa mita moja, lakini baadhi yalikuwa na ukubwa wa kupitisha magari na yalichimbwa kwenda chini zaidi, na kuwa na uwezo wa kuhimili mashambulizi ya Israel.

Umoja wa Mataifa umezilaumu pande zote mbili Israel na Hamas kuwa zimefanya uhalifu wa kivita katika mzozo huo.

Akizungumza juzi katika mpaka wa Rafah Mkuu wa Haki za Binadamu wa umoja, Volker Türk alisema ukatili ambao ulifanywa na makundi ya wapiganaji wa Kipalestina Oktoba 7 ulikuwa mbaya, wa kikatili na wa kushtua.

Alisema, adhabu ya pamoja inayofanywa na Israel dhidi ya raia wa Palestina pia ni sawa na uhalifu wa kivita, kama vile uondoaji wa nguvu usio halali wa raia.

Türk alielezea shambulio la mabomu katika Ukanda wa Gaza linasababisha madhara makubwa kwa maisha ya binadamu.

Wakati huo huo, Italia ilisema imepeleka meli yenye hospitali karibu na pwani ya Gaza ili kusaidia kuwatibu majeruhi.

Waziri wa Ulinzi wa Italia, Guido Crosseto alisema meli hiyo imeondoka juzi kutoka bandari ya Civitaveccia, magharibi mwa Italia ikiwa na watumishi 170, ambao ni pamoja na watu waliofunzwa kutoa huduma za dharura.

Meli hiyo itasimama Cyprus kabla ya kuelekea kwenye eneo lililo karibu zaidi na Ukanda wa Gaza, na majeruhi watapelekwa kwenye meli hiyo na kutibiwa kisha watarudishwa eneo hilo.

Kulingana na Waziri Crosetto hiyo ni operesheni ya kwanza ya aina yake ya kiutu kufanyika katika eneo hilo na anaamini mataifa mengine yatafuata nyayo zao.

Katika hatua nyingine, Uholanzi ilisema itapeleka meli ya kijeshi katika eneo la Cyprus kusaidia utoaji wa misaada ya kiutu katika Ukanda wa Gaza.

Waziri wa Ulinzi wa Uholanzi, Kajsa Ollongren alisema meli hiyo pia inaweza kusaidia kuwaokoa watu.

Mapigano hayo yanazidi kuwaathiri Wapalestina ambao kwa sasa wana uhitaji mkubwa wa maji, chakula, madawa na makazi mapya, baada ya Israel kuendelea kuharibu miundombinu kwa kushambulia kwa mabomu Ukanda wa gaza.

Katika hatua nyingine, taarifa zinaeleza mpaka wa Rafah bado umefungwa mpaka jana asubuhi.

Uongozi wa Hamas walisema wanataka watu waliojeruhiwa kuruhusiwa kuvuka mpaka huo kwenda nchini Misri kabla ya raia zaidi wa kigeni kuruhusiwa kuondoka.

Kituo cha mpakani kati ya Gaza na Misri kinatumika kuingia kwa misafara ya misaada na kutoka raia wa kigeni na watu waliojeruhiwa kwenda Misri.

Hamas walisema mpaka huo umjemefungwa kwa sababu ambazo hazijathibitishwa.

**DW**

## Marekani yashambulia Syria

**WASHINGTON, Marekani**

WAZIRI wa ulinzi wa Marekani, Lloyd Austin amesema ndege za kivita za Marekani zimeshambulia ghala la silaha katika eneo linalohusishwa na nchi ya Irani lililopo Syria.

Eneo hilo ambalo liko mashariki mwa Syria, lilishambuliwa na Marekani juzi kulipiza kisasi cha mashambulizi dhidi ya wanajeshi wake.

Austin alisema kwenye taarifa yake kwamba wanajeshi wa Marekani walifanya shambulizi la kujilinda katika kambi yake, mashariki mwa Syria baada ya wanajeshi wake kushambuliwa nchini Iraq na Syria.

Alisema, nchi yake ilijiandaa kikamilifu kuchukua hatua zaidi za kuwalinda watu wake pamoja na kambi zao.

Hii ni mara ya pili katika kipindi cha wiki mbili kwa Marekani kulenga maeneo kama hayo nchini Syria.

**DW**

## Serikali ya Ethiopia, waasi wajadili amani Tanzania

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

SERIKALI ya Ethiopia na kundi la waasi la Oromo Liberation Army (OLA) wanafanya mazungumzo nchini Tanzania kujaribu kumaliza uasi uliodumu kwa miaka mitano.

Jimbo la Oromo linaongoza kuwa na idadi kubwa ya watu nchini humo.

Kundi hilo ambalo serikali inaliona kama shirika la kigaidi, limekuwa likipigana tangu 2018, baada ya kujitenga na Oromo Liberation Front (OLF)baada ya kuachana na mapambano ya silaha.

Chanzo kimoja cha kidiplomasia kinaeleza kwamba mazungumzo yamekuwa yakiendelea kwa muda wa siku 10 takriban siku kumi.

Mazungumzo hayo yanaelezwa yanakwenda vizuri "Pande zote mbili zina matumaini ya kufikia makubaliano." Kilisema chanzo hicho Duru ya awali ya mazungumzo,iliyofanyika mwishoni mwa Aprili na mapema Mei, ilimalizika bila kupata makubaliano yoyote.

Ingawa pande zote mbili zilionyesha nia ya kuendelea na majadiliano, OLA baadaye ilishutumu serikali kwa kuanzisha mashambulizi dhidi ya waasi, na kueleza kwamba ni kinyume na nia njema ya kuzuia na uhasama.

Kabila la Oromo,linaongozwa kwa ukubwa nchini Ethiopia na kwa muda mrefu limekuwa likilalamika kutengwa.

Tangu OLA ilipojitenga na OLF na kuanza mapigano, msururu wa makundi yenye silaha yameibuka huko Oromia yakidai kuwa sehemu ya harakati zake.

# JKU SC YAITANGAZIA VITA MLANDEGE LIGI KUU ZBAR

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

VITA ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar inatarajia kuendelea kwa Maafande wa JKU SC kuwakaribisha Mlandege katika mechi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mau A visiwani hapa.

JKU yenye pointi 20 ndio vinara wa ligi hiyo wakati wapinzani wao wa karibu ni KVZ FC yenye alama 19 na nafasi ya tatu inashikiliwa na Zimamoto yenye pointi 17.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa JKU, Salum Ali, alisema anakutana na timu nzuri ambayo imesheheni wachezaji vijana wanaocheza kwa umakini kwa ajili ya kusaka ushindi.

Ali, alisema wamejiandaa vizuri kuwakabili wapinzani wao na amewaandaa nyota wake kuonyesha kiwango bora lakini kuzidisha umakini wa hali ya juu wakati wote wa mchezo.

Aliongeza anatarajia kupanga kikosi kitakachoingia kutafuta matokeo mazuri ili kuendelea kujiimarisha katika kilele cha msimamo wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kuelekea mchezo huu timu yangu imefanya mazoezi mbalimbali ikiwamo kufanyia kazi makosa kadhaa niliyoyaona katika michezo iliyopita hasa katika upande wa mabeki wa kulia.

Tutashuka dimbani kukutana na timu nzuri yenye wachezaji wengi vijana ambao bado wanahamu ya kucheza soka, lakini pia tunacheza na timu ambayo inahamasishwa zaidi na mashabiki wao nje ya uwanja hivyo ni lazima tuwe makini ili kupata alama tu," alisema kocha huyo.

Kocha Msaidizi wa Mlandege FC, Jaala Abdallah, alisema wanaenda kucheza na timu ambayo tayari imeonyesha nia ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu, hivyo mchezo wowote kwao ni kama fainali.

Abdallah alisema, katika mchezo huo wachezaji wake wanatakiwa kuongeza umakini na kutokuwa na hofu au papara ya aina yoyote ili kuvuna alama tatu.

Alisema lengo la Mlandege ni kuhakikisha wanamaliza mzunguko wa kwanza wakiwa katika nafasi nne za kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar.

Mlandege yenye pointi 14 iko katika nafasi ya nane katika msimamo wa ligi hiyo inayodhaminiwa na PBZ.



Mshambuliaji wa JKT Queens, Stumai Abdallah (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Athletico Abidjan katika mechi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake iliyochezwa kwenye Uwanja wa Manispaa wa Mji wa Korhogo Ivory Coast, juzi usiku. JKT Queens ilipata ushindi wa mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# Vishale waahidi ubingwa Kenya

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Vishale imewasili salama Kenya na imetamba imejipanga vyema kuhakikisha inapeperusha vizuri bendera ya Tanzania katika mashindano ya Afrika Mashariki yatakayoanza jijini, Nairobi imeelezwa.

Mashindano hayo yanashirikisha timu kutoka Tanzania, Uganda, Burundi, Rwanda na wenyeji Kenya.

Wachezaji wanaounda kikosi cha Tanzania ni pamoja na Noah Isaya, Yohana Kisau, Joachim Mollel, John Mlay, Modah Happens na Irene Kihupi.

Akizungumza na gazeti hili jana, nahodha wa timu hiyo, Mollel alisema wamefanya maandalizi mazuri na kazi iliyobakia ni kupambana kusaka ubingwa.

"Tumefanya maandalizi mazuri, tunaenda kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania kwa kushinda na si kushiriki, kikubwa Watanzania watuombee dua ili tufanye vizuri katika mashindano hayo, tunataka turudi nyumbani kifua mbele," alisema Mollel.

Ofisa wa Michezo Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Charles Maguzu, amewataka wachezaji wa timu hiyo kuonyesha uzalendo kwa kupambana katika mashindano na kurejea nyumbani na ushindi.

"Licha ya kupata nafasi ya kwenda katika mashindano haya na kuahidi kufanya vizuri, ninawakumbusha viongozi wa mchezo huu kuupeleka katika ngazi ya shule," alisema Maguzu.

## Chabruma aiweka JKT Queens pazuri

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya wenyeji Athletico Abdijan, Kocha Mkuu wa JKT Queens ,Esther Chabruma, amesema matokeo hayo yamefufua matumaini ya kusonga mbele katika mashindano hayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake yanayoendelea nchini Ivory Coast.

JKT Queens ilipata kichapo cha mabao 2-0 katika mechi ya kwanza ya hatua ya makundi kutoka kwa mabingwa watetezi, Mamelodi Sundowns Ladies ya Afrika Kusini.

Chabruma aliliambia Nipashe ushindi uliopatikana katika mechi hiyo ya juzi usiku waliutafuta kwa 'udi na uvumba' na sasa ili kuwarudisha tena kwenye mbio za kufuzu hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo yanayofanyika kwa mara ya tatu.

Kocha huyo amewapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha mchezo mzuri na ameongeza wanarejea kwenye uwanja wa mazoezi ili kujipanga na mchezo wa tatu ambao watakutana na Sporting Casablanca ya Morocco.

Alisema mchezo huo ni muhimu kupata ushindi kwa sababu ndio unawapa nafasi ya kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Ninamshukuru Mungu kwa kupata matokeo mazuri, ninawapongeza wachezaji wangu kwa kupambana na kujituma, ushindi huu wa mabao 2-1 ni faraja sana kwetu, umerejesha morali kwa kila mmoja wetu.

Mchezo ulikuwa mgumu sana kwa sababu wapinzani wetu walitangulia kupata bao la kwanza na vijana wangu wakajitoa na kuhakikisha wanafanikiwa kusawazisha na kuongeza la pili, " alisema nyota huyo wa zamani wa Twiga Stars.

Aliongeza kwa sasa wamesahau matokeo ya mechi iliyopita na wanajiimarisha kusaka pointi tatu ili watimize malengo ya kurejea nyumbani na ubingwa.

"Mechi ya kwanza tulipoteza na Mamelodi Sundowns walituzidi katika uzoefu kwa sababu wenzetu wako kwenye haya mashindano kwa misimu mitatu, baada ya mchezo huo nikarudi kwenye uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu yetu na hatimaye tumepata ushindi mbele ya wenyeji Athletico d'Abidjan.

Sasa tunaendelea kukisuka kikosi kujiandaa na mchezo ujao dhidi ya Sporting Casablanca, tunahitaji ushindi ili kusonga mbele, ninaamini tutacheza nusu fainali," Chabruma alisema.

Mamelodi Sundowns Ladies yenye pointi sita ndio vinara wa Kundi A wakifuatiwa na JKT Queens yenye pointi tatu, Athletico d'Abidjan na Sporting Casablanca kila mmoja ana pointi moja.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### EZE, CRYSTAL SAFI
MSHAMBULIAJI wa wa England, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 25, anakaribia kukubali mkataba mpya utakaomfanya alipwe pauni 100,000 kwa wiki na Crystal Palace baada ya kuafikiana kimsingi na klabu hiyo. **(Mail)**

### 'WIRTZ HAENDI KOKOTE'
BAYER Leverkusen inasisitiza kiungo wa kati wa Ujerumani, Florian Wirtz mwenye umri wa miaka 20, hataondoka katika klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani ifikapo Januari, huku Mkurugenzi Mkuu, Simon Rolfes akikana Liverpool tayari wamewasilisha ombi la pauni milioni 85. **(Kicker)**

### SANCHO KUONDOKA UNITED
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23 anatarajiwa kuondoka Manchester United katika dirisha dogo la Januari. **(Fabrizio Romano)**

### MADRID YAMKATAA MBAPPE
KLABU ya Real Madrid haina mpango wa kumsajili fowadi wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24, hata iwapo ataamua kutoongeza mkataba wake na Paris St-Germain na kuondoka bila malipo msimu ujao. **(Cadena SER)**

### NEWCASTLE YASAKA VIUNGO
KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe ameonyesha nia ya kuimarisha safu yake ya kati katika dirisha la uhamisho la Januari, huku Kalvin Phillips wa Manchester United mwenye umri wa miaka 27 na Mchezaji wa kimataifa wa Ureno, Ruben Neves (26), wakiwa katika mipango yake **(The I)**

### UNITED YAJIPANGA JANUARI
KLABU ya Manchester United italazimika kufanya mikataba ya bei ya chini au ya mikopo katika dirisha la usajili la Januari huku kukiwa na sintofahamu juu ya umiliki wao. **(Mail)**

### EDWARDS ATAJWA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur imeonyesha nia ya kumsajili tena mshambuliaji wa England, Marcus Edwards, ambaye alipitia chuo chao cha mafunzo ya chipukizi na sasa anachezea Sporting Lisbon ya Ureno. Lakini Chelsea pia wanavutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. **(Correio de Manhao)**

### CRESPO KUTUA SAUDIA
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Chelsea na Argentina, Hernan Crespo mwenye umri wa miaka 48 anatazamiwa kutangazwa kocha mkuu mpya wa klabu ya Al Ain inayoshiriki Ligi ya Saudia. **(Mail)**

### BAYERN, ARSENAL VITANI
KLABU ya Bayern Munich itapambana na Arsenal katika harakati za kuwania huduma ya kiungo wa kati wa Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 24 kutoka Real Sociedad **(Bild, Mirror)**

### XAVU KUBAKIA BARCA
BARCELONA inamuunga mkono Kocha wake, Xavi mwenye umri wa miaka 43 licha ya klabu hiyo kushuhudia kudorora kwa hali ya mchezo wao. **(ESPN)**

### CASEMIRO ANUKIA SAUDIA
KIUNGO wa kati wa Manchester United na Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 31 analengwa na timu za Saudia katika dirisha dogo la Januari. **(90min)**

## DON... A SOKA MAGA... A ULAYA



# KANE AFURAHIA YEYE KUNG'ARA NA BAYERN

**Afunga mawili na kuipeleka timu hiyo 16 bora Ulaya mapema huku...**

**MUNICH, Ujerumani**

HARRY Kane amekiri Bayern Munich wanafurahia kupata mafanikio mapema katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya lakini anafahamu kutakuwa na changamoto kali zaidi mbeleni.

Kane alifunga mabao mawili dakika za lala salama wakati Bayern Munich ikiilaza Galatasaray 2-1 na kufuzu kwa hatua ya 16 bora.

Nahodha huyo wa England aliendelea na kiwango chake kizuri cha kufunga mabao, na sasa amepata goli la kushangaza na kufikisha mabao 19 katika mechi 15 kwenye mashindano yote msimu huu.

Kane aliiambia UEFA: "Tumemaliza kileleni katika kundi rasmi jambo ambalo ni zuri. Nadhani inaonyesha ni wapi tunataka kuwa kama timu.

"Tulikuwa na michezo miwili migumu sana ya ugenini huko Copenhagen na Galatasaray pia, kwa hivyo kuanza kundi na ushindi mara nne kati ya nne na kumaliza kileleni tayari ni shukrani kwa wachezaji wote.

"Tunaweza kufurahia lakini tunajua mwisho wa biashara ni hatua ya mtoano."

Kane mwenye umri wa miaka 30 alidokeza ilikuwa ni suala la muda kabla ya Bayern Munich kufuzu kwa hatua hiyo.

Aliongeza: "Katika kipindi cha kwanza, tuliingia katika nafasi ya tatu ya mwisho tulikosa pasi ya mwisho au umaliziaji wa mwisho. Tulijua katika kipindi cha pili tulibaki na kasi hiyo.

"Tuliingia kwenye maeneo hatari vizuri kipindi cha kwanza, kitu pekee kilikosekana ni pasi ya mwisho.

"Tulifanya vyema zaidi katika kipindi cha pili. Nina furaha tulifuzu kwa hatua ya mtoano.

"Kama mshambuliaji, napenda kufunga mabao, kuwa uwanjani na kushinda. Nina furaha sana kuisaidia timu na nina furaha kuwa hapa."

Ushindi huo unamaanisha Bayern Munich wanaongoza Kundi A wakiwa na pointi 12 huku Galatasaray wakiwa nafasi ya tatu sawa na Copenhagen, ambao waliwafunga Manchester United magoli 4-3.

Vijana hao wa kocha Thomas Tuchel watawakaribisha Copenhagen kabla ya kuelekea Old Trafford.

# ANDRE WA FLUMINENSE AGOMBEWA EPL




**SAO PAULO, Brazil**

KLABU ya Fluminense inatarajia kumuuza kiungo wake nyota Andre katika dirisha la usajili la Januari huku kukiwa na nia kubwa na inayoongezeka kutoka katika timu za Ligi Kuu England, kwa mujibu wa 90min.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alikuwa sehemu muhimu wakati wa ushindi wa Fluminense wa Copa Libertadores, na kushinda ubingwa huo wa Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini kwa mara ya kwanza katika historia ya klabu hiyo dhidi ya Boca Juniors katika fainali iliyochezwa Jumamosi iliyopita.

90min iliripoti wakati wa majira ya joto Andre alikuwa amedhamiria kuona kampeni ya Fluminense ya Copa Libertadores na hivyo akapoteza nafasi ya kuelekea Ulaya, huku Liverpool wakimwona kama mbadala wa Romeo Lavia baada ya Mbelgiji huyo kuchagua Chelsea.

Vyanzo vilivyo karibu na Fluminense vimeiambia 90min wanatarajia Andre kuhamia Ulaya kwa muda mrefu katika dirisha lijalo la usajili, ingawa mazungumzo hayajafanywa na klabu yoyote kuhusu makubaliano hivi sasa.

Liverpool wanapanga kumsajili Januari na, ingawa bado wanavutiwa na Andre, hawajazungumza na kiungo huyo tangu msimu wa joto.

Fulham pia wanamtaka Andre kwa muda mrefu na wamejaribu mara mbili kumsajili huko nyuma.

Bado yuko kwenye rada zao kama mbadala wa Joao Palhinha, ambaye bado analengwa na Bayern Munich.

Arsenal pia imekuwa ikimfuatilia Andre na anathaminiwa sana na Mkurugenzi wa Michezo, Edu na yuko kwenye orodha yao fupi kabla ya dirisha la Januari.

Kuvutiwa na Andre kumeongezeka katika wiki za hivi karibuni, huku Tottenham Hotspur, Juventus, Napoli na Lyon zikimtafuta katika hatua za mwisho za mbio za Fluminense za Copa Libertadores.

Andre amecheza mara mbili na timu ya wakubwa ya Brazil na ameitwa kwenye kikosi cha Fernando Diniz kwa ajili ya mechi zao za kimataifa za Novemba dhidi ya Colombia na wapinzani wao Argentina.

## Bruyne, Osimhen kutimkia Saudia

**RIYADH, Saudi Arabia**

KUNA uwezekano mkubwa kwa timu ya A-Etifag ya Saudi Arabia ikawasilisha ofa ya kuwasajili kwa pamoja Kevin de Bruyne wa Manchester City na Victor Osimhen wa Napoli katika dirisha lijalo la usajili wa majira ya baridi.

Taarifa hii imeibuka baada ya kocha wa wababe hao, Steven Gerrard kuthibitisha timu hiyo imepanga kuingia sokoni Januari kwa ajili ya kusajili mastaa mbalimbali kutoka Barani Ulaya.

Katika dirisha lililopita la majira ya kiangazi A-Etifaq ilifanikiwa kuwasajili Jordan Henderson, Georginio Wijnaldum na Damarai Gray, lakini bado inataka kuendelea kumwaga mkwanja kwa ajili ya kunasa mastaa wengine.

Osimhen ambaye mkataba wake unamalizika 2025, aliwahi kuhusishwa na baadhi ya timu za Saudia Arabia katika dirisha lililopita la kiangazi, lakini mchakato ulishindikana.

Kwa upande wa De Bruyne, Manchester City inadaiwa kutohitaji kumsainisha mkataba mpya kutokana na hali yake ya majeraha ya mara kwa mara yanayomsumbua kwa sasa.




## Casemiro: Ninajuta kusajiliwa United



**MANCHESTER, England**

KIUNGO Casemiro, raia wa Brazil amesema anajuta kwa kufanya uamuzi wa kujiunga na Manchester United.

Casemiro alijiunga na United kwa mkataba wa pauni milioni 70 msimu uliopita wa joto na kumaliza safari yake ya miaka tisa ya kubeba mataji akiwa na Real Madrid.

Akiwa Hispania alishinda mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwenye safu ya kiungo akiwa pamoja na Toni Kroos na Luka Modric, ambapo watatu hao waliunda ushirikiano wa kutisha ambao kwa kiasi kikubwa.

Kuwasili kwa Mbrazili huyo United mwanzo kulisaidia kubadilisha timu ya Erik ten Hag katika msimu wake wa kwanza, na kuongeza usawa, udhibiti kwenye eneo la kiungo.

United walimaliza ukame wao wa miaka sita wa kutotwaa taji, na kisha wakabeba Kombe la Ligi 'Carabao Cup', huku pia ikifika fainali ya Kombe la FA na kumaliza katika nafasi tatu za juu kwenye Ligi Kuu England.

Hata hivyo kiwango cha Casemiro kimedorora msimu huu na maswali yameibuka juu ya nafasi yake kwenye kikosi hicho.

Sofyan Amrabat na Mason Mount wote walijiunga msimu huu wa joto ili kuongeza ushindani kwa nafasi ya kiungo.

Ripoti kutoka El Nacional sasa inaeleza jinsi Mbrazil huyo, ambaye ana mkataba wa muda mrefu United, sasa anajutia kubadilika kwa maisha yake kutoka Madrid mwaka mmoja uliopita.

## HABARI MICHEZO

# BARA, ZANZIBAR, UGANDA ZATINGA NUSU FAINALI U-15

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Soka ya Tanzania Bara ya vijana wa umri chini ya miaka 15 pamoja na 'ndugu' zao wa Zanzibar zimetinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-15), yanayoendelea kwenye Uwanja wa Njeru ulioko Jinja, Uganda.

Zanzibar imetinga hatua hiyo baada ya kuifunga Somalia mabao 4-0 wakati Tanzania Bara imewaadhibu Rwanda magoli 2-1.

Timu hizo zimesonga mbele baada ya kufikisha pointi sita, Zanzibar ikiwa kinara katika Kundi B kutokana na kuwa na idadi nzuri ya mabao ya kufungwa na kufuatiwa na Tanzania Bara.

Ndugu hao wawili wanatarajia kukutana kesho katika mechi ya kukamilisha hatua ya makundi na kupata kinara wa kundi hilo.

Mabao yote mawili ya Tanzania Bara yaliwekwa kimiani na Peter Arobagasti huku la kufutia machozi la Wanyarwanda lilipachikwa na Patrick Niyomugabo dakika moja kabla ya mechi kumalizika.

Zanzibar ambayo inaonekana tishio msimu huu katika michuano hiyo mabao yake yalifungwa na Mohamed Nassor, Salehe Abdallah, Luqman Othman na Hussein Mbegu.

Zanzibar ilianza vyema michuano hiyo kwa kuifunga Rwanda mabao 3-0 na mpaka sasa haijaruhusu bao lolote kwenye nyavu zao.

Baada ya mechi ya kesho, wawakilishi hao kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitajiandaa kucheza hatua ya nusu fainali dhidi ya timu zilizofanya vyema kutoka Kundi A linaloongozwa na Uganda.

Mashindano hayo yanafanyika chini ya usimamizi wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), ambayo iko chini ya Mwenyekiti wake, Wallace Karia kutoka Tanzania.

# Kibu kurejea dimbani mapema

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umesema hali ndani ya kikosi chao iko shwari na imeweka wazi mshambuliaji wao nyota, Kibu Denis, atarejea uwanjani mapema.

Kibu aliumia katika mechi dhidi ya watani zao, Yanga ambayo ilimalizika kwa Simba kupokea kichapo cha mabao 5-1, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumapili iliyopita.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema jana kila kitu kinakwenda vyema na wanafurahi wachezaji ambao walikuwa na majeraha wameimarika na wakati wowote wataanza kuitumikia timu hiyo.

Kajula alisema kila mchezaji wa Simba anaonyesha yuko tayari kuendelea na mapambano kuhakikisha timu yao inatimiza malengo yake.

"Ninafurahi kuona kila kitu kinakwenda vizuri, wachezaji wote wanafanya mazoezi vizuri, hali ya wachezaji ambao walikuwa majeruhi inaleta faraja, wote watarejea mapema uwanjani.



Bado tunaendelea kujipanga kwa ajili ya kuhakikisha tunapata ushindi katika mechi zote zilizoko mbele yetu, hakuna kitakachoshindikana," Kajula alisema hayo jana kabla ya kuelekea uwanjani kuivaa Namungo.

Baada ya mechi ya jana, Simba itaendelea na maandalizi yake kwa ajili ya kuikaribisha ASEC Mimosas katika mchezo wa hatua ya makundi wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa Novemba 25, mwaka huu.



Mshambuliaji wa Timu ya Soka ya vijana wa umri chini ya miaka 15 ya Tanzania Bara, Juma Kaniki (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Rwanda katika mashindano ya CECAFA U-15 iliyochezwa kwenye Uwanja wa Njeru, Uganda juzi. Bara ilishinda mabao 2-1. **PICHA: TFF**

# Aiyee, TMA mambo safi Championship

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI TMA FC inaongoza katika Ligi ya Championship hadi kufikia raundi ya tisa, straika wa Mbuni, Salim Aiyee, anaendelea kuwachachafya wenzake katika orodha ya ufungaji bora baada ya kufikisha mabao sita.

Aiyee, nyota wa zamani wa Stand United wakati huo ikiwa Ligi Kuu Tanzania Bara na KMC, amefikisha magoli sita huku timu yake ya Mbuni yenye pointi 15 ikiwa katika nafasi ya sita katika msimamo wa ligi hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa jana na Bodi ya Ligi, wanaoshika nafasi ya pili katika orodha ya wafungaji ni Abdulkarim Segeja wa Copco, Edgar William (KenGold), Ramadhani Kapera, Maulid Khalid (Mbeya Kwanza), Kassim Shaibu (Green Warriors), wote wamepachika mabao matano.

Mastraika waliofunga mabao manne ni Herbert Lukindo wa Biashara United, Mishamo Daud (KenGold) na Kika Salum wa Pan African ya Dar es Salaam.

Katika msimamo wa ligi hiyo iliyoko raundi ya tisa, TMA yenye maskani yake jijini Arusha inaongoza ikiwa na pointi 21, KenGold ikiwa ya pili na pointi 20 mkononi wakati Mbeya Kwanza yenye pointi 20 inafuatia na Pamba FC ipo kwenye nafasi ya nne ikikusanya pointi 18.


Polisi Tanzania inakamata nafasi ya tano na pointi zake 16, Mbuni ni ya sita ikiwa na pointi 15 wakati nafasi ya saba inashikiliwa na Biashara United yenye pointi 12 sawa na Stand United ya mkoani Shinyanga.

Maafande wa Ruvu Shooting ambayo iliteremka daraja msimu uliopita wanaburuza mkia katika ligi hiyo wakiwa na pointi moja tu mpaka sasa, wamecheza mechi tisa.

Timu mbili zitakazomaliza katika nafasi ya juu katika ligi hiyo zitapanda moja kwa moja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, huku zile zitakazomaliza katika nafasi ya tatu na ya nne zitapambana kwenye mechi za mtoano za klabu za Ligi Kuu.

Ligi ya Championship zamani Ligi Daraja la Kwanza ndio ligi ya pili kwa ukubwa kwa upande wa Tanzania Bara ikifuatiwa na First League .

Michezo
Ijumaa Novemba 10,
Nipash



Kane afurahia yeye kung'ara na Bayern

UKURASA 21




Kiungo wa Simba, Clatous Chama (kushoto), akijiandaa kumtoka nyota wa Namungo FC, Frank Domayo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA, NAMUNGO ZAGAWANA POINTI

●●●Bao la Baleke lawanusuru Wekundu wa Msimbazi kupata kipigo cha...

**Na Adam Fungamwango**

BAO la kusawazisha lililofungwa na straika, Jean Baleke liliinusuru Simba kupata kipigo cha pili mfululizo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana.

Matokeo hayo yanaifanya Simba ifikishe pointi 19 na kubakia pale pale kwenye nafasi ya tatu ikizidiwa mabao ya kufunga na Azam FC iliyoko nyuma ya vinara Yanga yenye pointi 24.

Baleke alifunga bao hilo dakika ya 75 na kumfanya afikishe magoli saba katika Ligi Kuu Tanzania Bara, sawa na mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki.

Reliants Lusajo aliipatia Namungo bao dakika ya 28, akiuweka mpira nyavuni huku akimtazama kipa Ayoub Lakred, na kuwaacha wachezaji wa Simba wakiwa wamejilundika sehemu moja.

Ulikuwa ni mpira wa kona uliooshindwa kuokolewa na mabeki wa Simba, ukarudishwa kwa kichwa na Frank Domayo, kabla ya kumkuta sraika huyo aliyeukwamisha wavuni likiwa ni bao lake la pili msimu huu na la nane kwa timu hiyo.

Simba imecheza kwa mara ya kwanza chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Daniel Cadena na msaidizi, Selemani Matola baada ya aliyekuwa Kocha Mkuu, Roberto Oliveira kutimuliwa baada ya kipigo cha mabao 5-1 kutokwa kwa watani zao, Yanga.

Dakika ya tano baada ya mchezo kuanza Simba ilifika katika lango la Namungo kwa gonga safi za Clatous Chama na Saido Ntibazonkiza kabla ya pasi ya mwisho kuwekewa, Willy Onana, lakini shuti lake la mguu wa kushoto lililotoka nje.

Mohamed Hussein alikaribia kuipatia Simba dakika ya 13 baada ya kuwatoka wachezaji wa Namungo akiwa mita 30 aliachia shuti kali lililotoka juu kidogo ya lango na dakika sita baadaye, kipa wa Namungo, Jonathan Nahimana alifanya kazi ya ziada kwa kuruka juu na kupangua kwa ustadi mpira wa kichwa uliopigwa na Baleke.

Mkongomani huyo pia alikosa bao la wazi dakika ya 23 akiwa ana kwa ana na Nahimana, lakini alijichanganya na kupiga shuti dhaifu la juu, ukadakwa kirahisi.

Namungo ilifanya shambulizi la kwanza dakika ya 25 ambalo nusura liwapatia bao kupitia kwa Hamad Majimengi aliyepewa pasi mpenyenzo na Lusajo, lakini mpira ukatoka kidogo nje ya lango.

Simba baada ya mabadiliko ya kuwatoa Chama na Saido, wakiingia Moses Phiri na Shaaban Chilunda, akitoka pia Onana na kuingia Luis Miquissone waliisaidia kwa kiasi kikubwa kutawala mpira na hatimaye kufunga bao la kusawazisha.

Baleke alimalizika kazi nzuri iliyofanywa na Phiri aliyeondoka na mpira wingi ya kulia na kupiga krosi ya chini na mfungaji huyo kuunganisha.

Namungo nayo ilimtoa mfungaji, Lusajo na Domayo, wakiingia Shiza Kichuya na Kelvin Sabato, pia Pius Buswita alitoka nafasi yake ikachukuliwa na Saydou Blanche na ulikuwa ni mkakati wa kuhakikisha inalinda sare hiyo na ikafanikiwa.

Mabeki wa Namungo, Erasto Nyoni, Derick Mukombozi, Emmanuel Asante na Hassan Kibailo, walikaa imara kuhakikisha Simba haipati bao la pili baada ya kufanikiwa kusawazisha.

Namungo imefikisha pointi nane baada ya kucheza michezo tisa na kupanda hadi nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

## Gamondi afunguka ubora wa Coastal

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi ameweka wazi mechi dhidi ya Coastal Union ilikuwa ngumu tofauti na alivyokuwa akiifikiria, lakini amefurahi kupata ushindi katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa jijini, Tanga juzi.

Yanga imeendelea kukaa kileleni ikiwa na pointi 24 wakati Coastal Union bado inaandamwa na bundi kwa kubakia na pointi zao saba.

Gamondi aliliambia gazeti hili ushindi walioupata unaendelea kuwaweka katika nafasi nzuri ya kutimiza malengo yao ya kutetea ubingwa wanaoushikilia.

Kocha huyo alisema wanatambua wana kazi kubwa katika mechi zao zote wanazocheza kwa sababu wanahitaji kupata ushindi kwa kubadili mbinu kulingana na mchezo husika.

Alisema wamefanikiwa kupata pointi sita katika michezo miwili mfululizo, na aliweka wazi wanacheza kulingana na aina ya mpinzani ambaye anakutana nao.

"Tunatambua namna ushindani ulivyo, hilo lipo wazi hivyo tunaingia uwanjani tukiwa na mpango kazi wa kusaka ushindi, kikubwa ni kuona tunacheza vizuri na kuwapa burudani mashabiki wetu wanajitokeza uwanjani. Waendelee kuwa pamoja na sisi, kazi bado ipo na tunaamini tutafanya vizuri," alisema Gamondi.

Aliongeza kwa kuwapongeza wachezaji wa Coastal Union kwa kuonyesha kiwango kizuri huku akiwasifia zaidi idara ya ulinzi kwa kucheza kwa nidhamu muda mwingi wa mchezo huo.

"Niwapongeze vijana walipambana kwa sababu tulitoka kwenye mechi ngumu na kushinda mabao 5-1, baada ya siku mbili tulikuwa na mechi dhidi ya Coastal Union na kupata matokeo mazuri," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Naye nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, alisema kikosi chao kilikuwa na uchovu wa safari hali iliyosababisha mchezo huo dhidi ya Coastal Union kuwa mgumu.

Mwamnyeto alisema ilikuwa mechi ngumu lakini wanashukuru wamevuna pointi tatu muhimu ambazo zinaendelea kuwaimarisha katika msimamo wa ligi hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >